



## SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA, YA  
MHE. BURHAN SAADAT HAJI (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA  
MATUMIZI NA MAPATO YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, MIFUGO  
NA MAZINGIRA KWA MWAKA 2009/2010**

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA, YA  
MHE. BURHAN SAADAT HAJI (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA  
MATUMIZI NA MAPATO YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, MIFUGO  
NA MAZINGIRA KWA MWAKA 2009/2010**

**1.0 UTANGULIZI**

- 1.1** **Mheshimiwa Spika**, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2009/2010.
- 1.2** **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa uwezo wake kutujaalia uzima wa afya na nchi yetu kuwa ya amani na utulivu. Kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira napenda kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Alhaji Dk. Amani Abeid Karume kwa hekima na busara zake katika kuiongoza nchi yetu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa juhudini za kushajiisha na kusukuma maendeleo ya kilimo hapa nchini.
- 1.3** **Mheshimiwa Spika**, naomba kumpongeza Waziri Kiongozi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo Mheshimiwa Ali Juma Shamuhuna kwa michango na maelekezo yao wanayotupa katika kuimarisha sekta ya kilimo nchini.
- 1.4** **Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa juhudini zako kubwa unazozichukuwa kuliendesha vizuri Baraza lako tukufu ukisaidiana na Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu wa Baraza na Maofisa wa Baraza la Wawakilishi. Aidha, nawashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za kudumu za Baraza kwa michango yao, ushauri, maelekezo na mashirikiano yao mazuri na wizara yetu.
- 1.5** **Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira natoa mkono wa rambi rambi kwa ndugu wa marehemu na wananchi wa majimbo ya Magogoni - Unguja na Wawi - Pemba kwa vifo vya ndugu zetu Daudi Hassan Daudi na ndugu Soud Yussuf Mgeni. Vifo hivi vimeacha pengo kubwa kwa Baraza na Taifa kwa ujumla. Tunamuomba Mwenyeenzi Mungu awape subira wafiwa na azilaze roho za marehemu Mahala Pema Peponi - Amin.

- 1.6 **Mheshimiwa Spika**, vilevile naomba nitumie fursa hii kutoa mkono wa rambi rambi kwa jamaa wa wafanyakazi wetu wa Wizara waliofariki, kwa wavuvi waliopoteza maisha yao wakiwa katika shughuli zao za uvuvi pamoja na wasafiri waliofariki katika ajali ya kuungua kwa Jahazi la "AMANA PEMBA" na waliofariki kwa kuzama Meli ya M.V Fatihi. Aidha, kwa niaba ya Wizara pia natoa mkono wa rambi rambi na pole kwa wakaazi wa Mbagala Dar es Salaam kwa kufiwa na ndugu zao na maafa waliyoyapata kutokana na miripuko ya mabomu iliyotokea hivi karibuni. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape subira wafiwa na walioathirika wapate uzima kwa haraka na Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi waliofariki wote - Amin.
- 1.7 **Mheshimiwa Spika**, pia naomba nichukue fursa hii kutoa pongezi kwa Kampuni ya PETRO DELL kwa kutoa fidia ya vifaa vyenye thamani ya Sh. 15,000,000 kwa wavuvi 11 (6 wamepewa fidia na 5 wamesaidiwa), wavuvi hao ni kutoka katika vijiji vya Fundo, Ukunjwi, Pujini na Ziwani ambao walikatiwa nyavu zao na meli iliyokuwa ikifanya utafiti huko Pemba. Vifaa hivyo ni pamoja na nyavu kamili na vifaa vyengine ambavyo viliharibiwa.
- 1.8 **Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa viongozi, wanachama na wapenzi wa CCM wa Jimbo la Kikwajuni kwa umoja na mashirikiano yao mazuri katika kufanikisha vizuri maendeleo ya jimbo.

## 2.0 HALI YA KILIMO NA UZALISHAJI NCHINI

### 2.1 Sekta ya kilimo na uchumi

- 2.1.1 **Mheshimiwa Spika**, mchango wa sekta ya kilimo katika pato la Taifa umekuwa kwa asilimia 3.3 kutoka asilimia 27.3 kwa mwaka 2007/2008 hadi asilimia 30.8 kwa mwaka 2008/2009, ambapo mazao ya kilimo yamechangia asilimia 21.5, uvuvi 5.2, mifugo 4.6 na misitu 0.3. Aidha, sekta ya kilimo bado inaendelea kuwa sekta muhimu kiuchumi na inakadiriwa kuchangia wastani wa asilimia 75 ya mapato ya fedha za kigeni. Pamoja na hayo uchambuzi uliofanywa na tafiti mbalimbali unaonesha kwamba sekta ya kilimo bado ni mhimili mkuu wa maisha ya wananchi walio wengi kutoana na mchango wake wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha na kuwa na uhakika wa chakula na lishe. Hivyo, ni dhahiri kuwa kukua kwa sekta ya kilimo kutawanufaisha wananchi walio wengi hapa visiwani na kukuza uchumi kwa ujumla.

## **2.2 Hali ya uzalishaji**

- 2.2.1 Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa uzalishaji wa mazao ya chakula takwimu zinaonesha kuwa kuna ongezeko la uzalishaji wa mazao hayo la asilimia 5.7 kwa mwaka 2008/2009 ikilinganishwa na mwaka 2007/2008. Ongezeko hili limechangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mpunga, ndizi, viazi vitamu na majimbi. Hata hivyo, yapo baadhi ya mazao ambayo yameripotiwa uzalishaji wake kushuka mfano muhogo, mahindi na viazi vikuu. (**Kiambatanisho 1**).
- 2.2.2 Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea na jitihada za kuendeleza Sekta ya Mifugo lengo kuu ni kuwa na mifugo ya kisasa na yenye ubora na viwango vinavyokubalika kimataifa. Katika kufikia hili Wizara kupitia programu mbalimbali imekuwa ikiwapatia wakulima mbegu bora za mifugo, ikiwemo mitamba ya ngo'mbe wa maziwa, mbuzi wa maziwa na majogoo bora. Katika kipindi cha hivi karibuni jumla ya mitamba bora 764 ya ngo'mbe wa maziwa imetolewa kwa wafugaji na mbuzi wa maziwa wapatao 1,439 na majogoo bora 700 wametolewa katika vijiji mbalimbali vya Unguja na Pemba. Matarajio ni kwamba sekta hii itaendelea kukua hasa kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali, wafugaji na kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma mbalimbali za mifugo.
- 2.2.3 Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa samaki umeripotiwa kuongezeka kwa asilimia 9 kutoka tani 24,095 mwaka 2007 hadi tani 26,267 kwa mwaka 2008. Ongezeko hili limechangiwa zaidi na juhudzi za serikali za kutumia mbinu shirikishi katika kuhifadhi mazingira ya baharini na ukanda wa pwani, na kuwawezesha wavuvi wadogo kwa kuwapatia nyenzo na taaluma kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

## **2.3 Hali ya jumuiya za wazalishaji na mitaji katika kilimo**

- 2.3.1 Mheshimiwa Spika**, Udhifu wa jumuiya za wazalishaji na mitaji midogo ya kuekeza katika kilimo ni miiongoni mwa changamoto zinazokwamisha maendeleo ya Sekta ya Kilimo hapa nchini. Aidha, Wizara imekuwa ikifanya juhudzi mbalimbali za kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili ikiwa ni pamoja na kuimarisha jumuiya za wazalishaji pamoja na kushajiisha uanzishwaji wa vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo.
- 2.3.2 Mheshimiwa Spika**, uanzishwaji wa jumuiya za wazalishaji sambamba na vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo umekuwa ukihamasishwa katika

utoaji huduma mbalimbali za kilimo ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mfano kwa mwaka 2008 Idara ya Vyama vya Ushirika ilisajili vyama vya ushirika 327 vya miradi mbalimbali. Vilevile, Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji - PADEP ulianzisha vikundi 124, Programu ya kuimarisha huduma za kilimo - ASSP vikundi 200, Programu ya kuimarisha huduma za mifugo - ASDP-L vikundi 160, Mradi wa Uhifadhi wa Mazingira ya Ukanda wa Pwani - MACEMP vikundi 420.

**2.3.3 Mheshimiwa Spika**, lengo kuu katika kuimarisha jumuiya za wazalishaji ni kujenga uwezo wa kuongeza uzalishaji na kulinda maslahi yao kwa kuwafanya wawe na sauti moja katika kutetea haki zao hasa katika masuala ya masoko na udhibiti wa bei za mazao. Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo vinashajiishwa kwa lengo la kuwawezesha wazalishaji wadogo wadogo kupata na kuweza kuwekeza katika shughuli za uzalishaji.

**2.3.4 Mheshimiwa Spika**, mtizamo wa sasa wa Wizara katika kuendeleza kilimo ni:

- Kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo bora za kilimo, Mkakati ni kushirikisha wakulima, NGOs na sekta binafsi katika uzalishaji na usambazaji wa pembejeo hizo;
- Kuzijengea uwezo taasisi za wakulima ziweze kuongeza mitaji ya kuekeza katika shughuli za uzalishaji;
- Kuweka mazingira mazuri ya kisera na mfumo maalumu wa kusimamia masoko ya bidhaa za kilimo;
- Kuongeza kasi katika kutekeleza Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji;
- Kushajiisha suala la usarifu na kuongeza thamani ya mazao (value addition);
- Kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa wakulima, wafugaji na wavuvi pamoja na mafunzo kwa wafanyakazi kwa mujibu wa mahitaji ya Wizara.

## **2.4 Changamoto katika Sekta ya kilimo**

**2.4.1 Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua nzuri ya mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Kilimo, sekta hii bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zinarudisha nyuma kasi ya maendeleo. Changamoto hizo ikiwa ni pamoja na ongezeko la wizi wa mazao na mifugo, kukithiri kwa uchimbaji holela wa mchanga na ukataji ovyo wa miti, uvamizi wa maeneo ya kilimo kwa makaazi.

**2.4.2 Mheshimiwa Spika**, suala la uvamizi wa maeneo ya kilimo na kugeuzwa kuwa ya makaazi limekuwa sugu sana katika miaka ya hivi karibuni na linahatarisha kwa kiasi kikubwa hali ya usalama wa chakula nchini. Suala hili linapingana na azma ya Serikali yetu ya kuifanya Zanzibar kujitosheleze kwa chakula kwa vile uvamizi huu unaathiri moja kwa moja uzalishaji wa mazao ya chakula. Napenda kuchukuwa fursa hii kuziomba taasisi zinazohusika kufanya kazi kwa karibu na Wizara ya Kilimo katika kulitatua tatizo hili.

### **3.0 ATHARI ZA MTIKISIKO WA UCHUMI DUNIANI KATIKA SEKTA YA KILIMO**

**3.1 Mheshimiwa Spika**, Dunia hivi sasa imekabiliwa na changamoto kubwa ya kuporomoka kwa uchumi na soko la fedha hali ambayo imeathiri sekta za uzalishaji. Zanzibar kama nchi nyengine ulimwenguni imeanza kuathirika na hali hiyo katika sekta zake za uchumi ikiwemo kilimo. Kwa upande wa sekta ya kilimo mionganoni mwa athari zinazotarajiwaa kujitekeza ni :

- Kupungua zaidi kwa soko la mazao ya kilimo na kushuka kwa bei ya mazao yanayosafirishwa nje ya nchi hasa karafuu. Upungufu huu unatarajiwaa kupunguza mapato ya taifa na kipato cha wazalishaji;
- Kuongezeka kwa bei za pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea, mbegu bora na madawa ya wadudu waharibufu na magugu. Hali hii inatarajia kupunguza zaidi matumizi ya pembejeo bora za kilimo na kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya chakula;
- Kuongezeka kwa matumizi ya maliasili ikiwa ni njia mbadala kwa wakulima kujikimu kimaisha. Hali hii inaweza kurudisha nyuma jitihada za muda mrefu zilizofanywa na Selikali kwa kushirikiana na wananchi na wahisani katika kutunza maliasili zetu.

**3.2 Mheshimiwa Spika**, katika kuweka mazingira mazuri ya kukabiliana na athari za mtikisiko wa uchumi wa dunia, Wizara ya Kilimo imeshirikiana na Wizara ya Fedha na imeandaa waraka juu ya mikakati inayohitajika kutekelezwa ili kupunguza athari za mtikisiko wa uchumi wa dunia kwa Sekta ya Kilimo. Waraka huo umeunganishwa na waraka wa Tanzania bara ili kupata waraka mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupelekwa kwa wafadhili. Kwa ujumla mkakati huo umezingatia suala la kuongeza ruzuku ya serikali katika pembejeo na huduma za kilimo; kuongeza matumizi ya pembejeo na zana bora za kilimo; kuongeza vyanzo vya kimaisha kwa wazalishaji wadogo wadogo

(livelihood diversification); kuongeza ubora wa mazao yanayosafirishwa nje ya nchi.

- 3.3 **Mheshimiwa Spika** pamoja na matayarisho ya waraka huo, Wizara pia imeanza kuchukua hatua za haraka za kukabiliana na hali hiyo na tayari imeanzisha mpango maalumu wa kuzalisha mbegu ya mpunga ambayo baadae itasambazwa kwa wakulima. Katika awamu ya kwanza ya mpango huu jumla ya tani 300 za mbegu ya mpunga zilitarajiwa kuzalishwa. Hata hivyo kutokana na ukosefu wa mvua za kutosha kwa baadhi ya maeneo hivi sasa inakadirwa kuweza kupatikana tani 100 za mbegu ya mpunga msimu huu. Aidha, Wizara itaendelea kutoa ruzuku kwa pembejeo muhimu za uzalishaji.

#### **4.0 UTEKELEZAJI WA SERA NA MIKAKATI YA KUPUNGUZA UMASIKINI**

- 4.1 **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kusimamia na kutekeleza sera na mikakati ya kitaifa na kisekta kama njia mojawapo ya kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Mikakakti ya Wizara katika kutekeleza MKUZA imeelekezwa zaidi katika kupunguza umasikini wa kipato na kuongeza hali ya uhakika wa chakula na Lishe.
- 4.2 **Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha haya Wizara imeweka utaratibu maalumu kuhakikisha kwamba wazalishaji wenyewe kipato cha chini wanashiriki na kufaidika katika miradi ya maendeleo iliyo chini ya Wizara. Sambamba na juhud hizi, Wizara inaendela na juhud za kuweka mazingira ya kisheria ya kutekeleza Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Hivi sasa Wizara inatayarisha rasimu ya sheria (Food Security Bill) itakayopelekea kuundwa na kufanya kazi kwa Divisheni ya Uhakika wa Chakula na Lishe ndani ya Wizara ya Kilimo, ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji wa mipango ya Uhakika wa Chakula na Lishe.
- 4.3 **Mheshimiwa Spika**, Juhudi za Wizara katika kutekeleza sera na mikakati pia zimeelekezwa katika kuongeza huduma za elimu kwa wakulima kwa kutilia mkazo matumizi ya Skuli za Wakulima katika kueneza mbinu bora za uzalishaji, kuendeleza utafiti wa mazao ya chakula na biashara kwa lengo la kuongeza ubora wa mazao na kuongeza upatikanaji wa pembejeo bora za kilimo. Kwa mwaka 2008/2009 jumla ya Skuli za Wakulima 180 zimeanzishwa katika shehia mbalimblali za Unguja na Pemba ambapo wakulima na wafugaji 5,000 wameweza kufaidika na mafunzo hayo.

- 5.0 MPANGO MAALUMU WA KUENDELEZA ENEO LA MICHEWENI**
- 5.1** **Mheshimiwa Spika**, wizra yangu kwa kushirikiana na Serikali na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) inatekeleza mpango maalum wa kuendeleza eneo la Micheweni. Lengo ni kuwapunguzia umasikini wananchi wa Micheweni. Mkakati wa utekelezaji umelenga katika kuwajenga uwezo wananchi wa eneo hili waweze kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na kujajiri katika kazi mbalimbali zitakazowawezesha kujiongezea kipato
- 5.2** **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2008/2009 wizara ilitekeleza miradi sita ambayo kwa ujumla ilitumia Sh. 209,514,250 kuanzia Oktoba 2008 hadi Juni, 2009. Mchanganuo wa matumizi hayo kwa miradi ni kama ifuatavyo:-

Na	AINA YA MRADI	FEDHA ZILIZOTUMIKA SH
1	Mradi wa kuimarisha Kuku wa Kienyeji na ufugaji wa kuku wa kisasa	52,426,410
2	Mradi wa Ufugaji Nyuki	32,899,410
3	Mradi wa Utafiti wa Mbegu bora, wadudu waharibifu na uchunguzi wa udongo	38,523,300
4	Mradi wa Utunzaji wa Mwani	20,318,000
5	Mradi wa Ukarabati wa Miundombinu ya U/Maji - Saninga	49,910,000
6	Mradi wa Utumiaji Nishati Mbadala	14,069,500
<b>JUMLA</b>		<b>209,514,250</b>

- 6.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI MWAKA 2008/2009 NA MALENGO YA MWAKA 2009/2010**
- 6.1** **Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla utekelezaji katika Sekta ya Kilimo unalenga katika kutekeleza sera za kitaifa, Sera za Sekta na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, ambazo zote kwa pamoja zinalenga katika kuongeza uzalishaji wa mazao yenye ubora na tija, kuongeza ufanisi katika kazi za uzalishaji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira.
- 6.2** **Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kilimo kuitia taasisi zake kwa mwaka 2008/2009 pamoja na malengo ya mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-
- 6.3 IDARA YA SERA NA MIPANGO**
- 6.3.1** **Mheshimiwa Spika**, Idara hii ndio kiungo kikuu cha Wizara ikiwa na majukumu ya kusimamia na kuratibu taasisi za ndani na nje ya Wizara, kukuza

mashirikiano na taasisi za Serikali ya Muungano, Jumuiya za Kikanda na Washirika wa Maendeleo. Idara pia inasimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi, utayarishaji na uratibu wa sera, sheria, mikakati na programu za maendeleo, utumishi na mafunzo kwa wafanyakazi.

### 6.3.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2008/2009

- 6.3.2.1 **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2008/2009 Idara ilikusanya mapato ya jumla ya Shilingi **1,098,930,556** hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2009. Hii ni sawa na asilimia 157.74 ya lengo. Aidha, katika kufanikisha kazi za uratibu Idara ilizindua rasmi Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe tarehe 16 Oktoba, 2008 sambamba na sherehe za maadhimisho ya siku ya chakula duniani. Idara pia imeandelea kusimamia utayarishaji wa sera ya masoko ya bidhaa za kilimo, sera ya mifugo, sera ya misitu na sera ya ushirika. Sera hizi hivi sasa zimo katika hatua ya kuwasilishwa kwa wadau na kupata maoni yao.
- 6.3.2.2 **Mheshimiwa Spika**, jumla ya wafanyakazi 202 wa Idara mbalimbali ziliopo chini ya Wizara wamepatiwa mafunzo yakiwemo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi katika fani za kilimo, mifugo, uvuvi, utunzaji wa mazingira uongozi na udhibiti wa fedha (**Kiambatisho 2**). Idara pia imeratibu mafunzo juu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI kwa wafanyakazi na wazalishaji. Aidha, wafanyakazi 584 wa kutwa wamepatiwa ajira ya kudumu.
- 6.3.2.3 **Mheshimiwa Spika**, Idara inaendela kusimamia utekelezaji wa programu tano za maendeleo, taarifa za utekelezaji kwa mwaka 2008/2009 na malengo ya mwaka 2009/2010 yanaoneshwa katika viambatisho. Programu hizo ni:
- Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo-ASSP, madhumuni ya programu hii ni kuwawezesha wakulima kupata na kutumia utaalamu na teknolojia za kilimo ambazo zitaongeza uzalishaji na kumuongezea mkulima kipato na uhakika wa chakula (**Kiambatisho 3**)
  - Programu ya Kuimarisha Huduma za Mifugo -ASDP-L madhumuni ya programu hii ni kuwawezesha na kuwaendeleza wafugaji masikini ili kuinua hali zao za uzalishaji na kipato. (**Kiambatisho 4**)
  - Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe - FSNP Programu hii ina lengo la kupunguza umasikini na kuongeza uhakika wa chakula na afya bora ikilenga zaidi kaya ambazo ni masikini (**Kiambatisho 5**)
  - Mradi wa Usarifu wa Mazao ya Kilimo (agro-processing), programu ina lengo la kujenga uwezo wa wakulima juu ya usarifu wa mazao,

ujasiriamali na kutoa huduma za udhibiti wa ubora kwa bidhaa zinazozalishwa kwa lengo la kuongeza ajira na kipato kwa wazalishaji. **(Kiambatisho 6)**

- Programu ndogo ya kuhamasisha na kutoa mafunzo ya UKIMWI, programu ina lengo la kutoa elimu sahihi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI kwa wafanyakazi, wakulima, wavuvi, wafugaji pamoja na wanaushirika kwa lengo la kupunguza maambukizi ya VVU kwa wadau wa Sekta ya Kilimo. **(Kiambatisho 7)**

### 6.3.3 MALENGO YA MWAKA 2009/10

#### 6.3.3.1 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010 Idara itatekeleza malengo yafuatayo:-

- Kusimamia ukusanyaji wa mapato, lengo ni kufikia Sh. 1,429,900,000;
- Kuandaa mazingira mazuri ya utekelezaji wa Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo katika ngazi za Taifa, Wilaya na Jamii, kufanya tathmini ya upatikanaji wa Chakula kwa Unguja na Pemba na kuendelea na utayarishaji wa Sera ya Masoko ya Kilimo
- Kusimamia na kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na maliasili;
- Kusimamia utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Utafiti na Elimu kwa Wakulima wa Wizara (Research and Extension Master Plan)
- Kuendelea kusimamia programu na miradi ya ASSP, ASDP-L, Usarifu wa Mazao (Agro-processing) na Uhakika wa Chakula na Lishe.
- Kuendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwa mujibu wa mahitaji ya taasisi zilizo chini ya Wizara na;
- Kuratibu mashirikiano na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa katika utayarishaji na utekelezaji wa miradi;
- Kufuatilia upatikanaji wa hati miliki za mali za Wizara ikiwa ni pamoja na mashamba yote ya kilimo
- Kukamilisha taratibu za kuwa na Mpango kamilifu wa Maendeleo ya kilimo (Agriculture Sector Development Program - ASDP).
- Kutayarisha Mkakati wa kuliendeleza lililokuwa shamba la mifugo la Makurunge na kufuatilia upatikanaji wa hati miliki kwa shamba hilo.

## **6.4 KAMISHENI YA KILIMO, UTAFITI NA ELIMU KWA WAKULIMA**

**6.4.1 Mheshimiwa Spika**, Kamisheni ina majukumu matatu makubwa ya kutoa huduma za Elimu kwa Wakulima, kuendeleza shughuli za Utafiti wa mazao ya kilimo na kuhakikisha upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo.

### **6.4.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2008/2009**

#### **Huduma za elimu kwa wakulima**

**6.4.2.1 Mheshimiwa Spika**, katika kutoa huduma za elimu kwa wakulima kwa mwaka 2008/2009, Kamisheni ililenga kuelimisha, kushauri na kufikisha matokeo ya utafiti kwa wakulima na wazalishaji wengine. Katika kufanikisha hayo kazi zifuatazo zilifanyika:

- Utayarishaji na urushaji wa vipindi 36 vya redio na TV;
- Ilihamasisha wakulima 1,000 na kusambaza vipeperushi juu ya uzalishaji bora wa mpunga wa kutegemea mvua ;
- Ilitayarisha na kutoa mafunzo kwa Mabwana na Mabibi shamba 120 kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba juu ya udhibiti wa maradhi na wadudu wa embe na uzalishaji bora wa mbegu za nafaka;
- Ilitoa mafunzo kwa wakulima 5,780 juu ya mbinu bora za uzalishaji wa mazao na uhifadhi wa mazingira;
- Ilishajiisha uanzishwaji wa miradi ya usarifu wa mazao kwa vikundi vitano vipyta na kuziimarisha skuli za wakulima.

#### **Utafiti wa Mazao ya Kilimo**

**6.4.2.2 Mheshimiwa Spika**, Utafiti wa mazao ya kilimo unafanyika katika vituo vikuu vya utafiti vya Kizimbani na Matangatuani na vituo vyengine vidogo vidogo vilivyopo maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Aidha, tafiti nyengine hufanyika kwa kushirikiana na wakulima na wazalishaji katika maeneo yao (on farm research). Kwa ujumla tafiti zote zinalenga katika kuongeza uzalishaji, kudhibiti maradhi na wadudu waharibifu wa mazao na kutafiti mbegu bora zinazo himili ukame, maradhi na zenye uwezo wa kutoa mazao mengi.

**6.4.2.3 Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2008/2009 kazi zilizotekelawa katika utafiti wa mazao ya chakula na biashara ni kama ifuatavyo:

- Kitengo cha mazao ya mizizi kiliendeleza utafiti wa mbegu mbalimbali za muhogo, viazi vitamu na viazi vikuu katika vituo vya utafiti;
- Aina nne mpya za mbegu za muhogo (Kizimbani, Machui, Mahonda na Kama) zimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima 350 katika maeneo ya Machui, Mahonda, Kinduni na Kisauni kwa kutumia njia ya mkulima kwa mkulima na mfumo wa stakabadhi za malipo (seed voucher system). Mfumo huu unawahuisha wakulima masikini na humuwezesha mzalishaji kumpatia mbegu mkulima baada ya mkulima kukabidhi stakabadhi;
- Mbegu za aina mbalimbali za mazao zilikusanywa zikiwemo 61 za muhogo, 28 za viazi vikuu, 32 za viazi vitamu, 34 za migomba na 40 za mpunga kwa ajili ya kuhifadhi na kudhibiti mbegu za asili kwa matumizi ya tafiti za baadae;
- Utafiti wa majaribio umefanyika kwa aina 14 ya mbegu mpya za mpunga wa kutegemea mvua aina ya NERICA. Matokeo ya awali yanaonyesha kwamba mbegu tano kati ya hizo zinatafaa kupelekwa kwa wakulima kwa majaribio zaidi;
- Divisheni ya utibabu wa mimea imeendeleza utafiti wa wadudu waharibifu wa mazao ya mboga mboga na muhogo (Spiral white flies) kwa kutumia madawa ya asili na matokeo yameonesha kuwa uharibifu unaofanywa na wadudu hao umepungua kwa asilimia 50.
- Utafiti juu ya kudhibiti nzi wa embe nao pia unaendelea kwa kutumia mitego maalumu na matokeo ya awali yameleta matumaini ambapo jumla ya nzi milioni mbili wamekamatwa tokea kuanza kwa kazi hiyo mwezi Oktoba 2007. Mpango wa baadae ni kuongeza mitego mengine 3,000 na kufanya mitego yote kwa kazi hiyo kufikia 5,000. Inakadirikwa kuwa uharibifu wa matunda umepunguwa kwa asilimia 30 hadi hivi sasa.
- Utafiti wa zao la nazi uliendelea kwa kufanya utafiti wa kudhibiti bungu wa minazi katika mashamba ya wakulima Unguja na Pemba.
- Kamisheni pia imefanya maandalizi ya Mkutano wa Mwaka wa Utafiti. Lengo la mkutano huo ni kuwakutanisha watafiti mbali mbali wa kilimo katika kujadili masuala ya utafiti na kuweka mikakati mipy ya utafiti katika sekta yakilimo.

- 6.4.2.4 Mheshimiwa Spika**, Wizara inawapongeza sana wataalamu na wafanyakazi wa Maabara ya Kizimbani kwa kazi zao nzuri za Utafiti wanazozifanya pamoja na uvumbuzi wa aina nne za mbegu za Muhogo.

#### **Huduma za Pembejeo na Zana za Kilimo**

- 6.4.2.5 Mheshimiwa Spika**, Sera ya Kilimo imesisitiza ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za uzalishaji na usambazaji wa pembejeo. Hata hivyo, kutokana na ushiriki mdogo wa sekta binafsi, Wizara bado inaendelea kuwa mtoaji mkubwa wa huduma hizo kupitia Kitengo cha Mpunga na Pembejeo kilichopo chini ya Kamisheni. Huduma za pembejeo zinahusisha uzalishaji na usambazaji wa mbegu za mazao ya chakula na biashara na usimamiaji wa kilimo cha mpunga wa kutegemena mvua. Vilevile, huduma hizi pia huhusisha ununuzi na usambazaji wa mbolea na kutoa huduma za matrekta na zana nyengine za uzalishaji.
- 6.4.2.6 Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2008/2009 huduma za matrekta zimeimarika na maeneo mengi yameweza kulimwa kwa wakati. Jumla ya ekari 10,297 za mpunga wa kutegemea mvua zimelimwa ikiwa ni sawa na asilimia 92 ya lengo. Mafanikio haya yamepatikana kutokana na ongezeko la matrekta 12 yaliyonunuliwa hivi karibuni. Pamoja na hizo ekari 11,850.75 zimelimwa kwa mkono na ekari 28.25 zimelimwa kwa jembe la kukokotwa na Ng'ombe;
- 6.4.2.7 Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha kazi za utoaji wa huduma za pembejeo Unguja na Pemba, Kitengo cha Mpunga na Pembejeo kimezalisha na kusambaza kwa wakulima tani 13 za mbegu ya mpunga, tani 7.2 za mbegu ya mahindi na mazao ya jamii ya kunde. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 93.7 ya lengo. Aidha, kitengo pia kimenunua na kusambaza kwa wakulima tani 203 za mbolea ya kupandia na kukuzia.
- 6.4.2.8 Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji huu, Kamisheni pia ilisambaza jumla ya tani 39 za mbegu ya mpunga na tani nane (8) za mbegu ya mahindi ikiwa ni msaada kutoka Shirika la Chakula na Kilimo (FAO). Tani 26.5 za mbegu ya mpunga na tani nne (4) za mahindi ziligaiwa kwa wakulima Unguja na tani 12.5 za mpunga na nne za mahindi ziligaiwa kwa wakulima wa Pemba. Vilevile, FAO imeisaidia Serikali jumla ya tani 556 za mbolea (DAP Tani 60 na Tani 496 UREA) ambayo imeshasambazwa kwa wakulima.

**6.4.2.9 Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Utafiti Kizimbani kimeendelea na kuzalisha miche ya miti ya matunda na mazao mengine ya kudumu. Kwa mwaka 2008, jumla ya miche 7,000 ya mazao ya biashara imezalishwa na kuuziwa wakulima. Kati ya miche hiyo Mikungu Manga ni 1,500, Mihiliki 2,700, Midalasini 800, Mitangawizi 700, Manjano 500, Pilipili Manga 400, Mibuni 300, Mivanila 100 na Minazi 40,000.

**6.4.2.10 Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2008/2009, Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima ilisimamia utekelezaji wa Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (PADEP) ambao umeendelea kujenga uwezo wa wazalishaji katika kutambua matatizo yao ya kilimo, kubuni na kuandaa mikakati ya kuyatatu. Muhtasati wa utekelezaji wa mradi huu unapatikana katika (**Kiambatisho 8**).

#### **6.4.3 MALENGO YA MWAKA 2009/2010**

**6.4.3.1 Mheshimiwa Spika**; Kamisheni ya Kilimo kwa mwaka 2009/2010 itaendelea kutoa huduma za elimu kwa wakulima, kuendeleza kazi za utafiti wa mazao, uzalishaji na usambazaji wa pembejeo. Aidha, kwa upande wa huduma za elimu kwa wakulima, malengo kwa mwaka huo ni:

- Kutayarisha na kurusha vipindi 48 vya radio na TV vinavyohusiana na utekelezaji wa mipango ya Sekta ya Kilimo, kuchapisha vipeperushi 3,000 na kuandika makala 40 za mambo mbalimbali yanayohusiana na kilimo;
- Kutoa mafunzo kwa mabibi/mabwana shamba 120 juu ya maradhi ya mimea na mifugo;
- Kutoa elimu kwa wakulima 4,500 juu ya mbinu bora za uzalishaji, udhibiti wa wadudu waharibifu na maradhi ya mimea na mifugo;
- Kutoa elimu kwa wakulima 350 juu ya matumizi ya jembe la kukokotwa na ng'ombe na kuwapatia nyenzo kwa bei nafuu;
- Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo (PADEP) katika wilaya nne mpya na wilaya tano za awali;
- Kuendeleza kilimo cha maweni kwa kushajiisha uzalishaji wa mazao na mbegu zinazostahamili hali halisi ya ukanda wa maweni na kuwashamasisha wakulima juu ya uendelezaji wa kilimo cha zao la minazi;
- Kusambaza mitego 12,000 ya kudhibiti mafunza ya matunda, Unguja na Pemba;

**6.4.3.2 Mheshimiwa Spika;** katika kuendeleza kazi za utafiti wa mazao ya chakula na biashara malengo kwa mwaka 2009/2010 ni kama yafuatayo:

- Kufanya utafiti wa udongo kwa lengo la kutafuta viwango vipyta vyta mbolea kwa mazao mbalimbali ya kilimo
- Kukusanya mbegu mbalimbali za asili na za kigeni kwa mazao makuu ya chakula (germplasm collection and maintenance) na kuendeleza utafiti na uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya chakula yakiwemo mpunga, mazao ya mizizi, mboga mboga na migomba;
- Kuendelea kufanya utafiti na udhibiti wa wadudu waharibifu wa mazao “Spiral white flies”;
- Kuendeleza mashirikiano na taasisi nyengine za kimataifa katika kuyapatia ufumbuzi matatizo ya nzi wa matunda “fruit flies” na masuala mengine yanayohusu udhibiti wa maradhi na wadudu waharibifu;
- Kuendeleza utafiti na uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya biashara yakiwemo mazao ya viungo, minazi na mengineyo;
- Kuendeleza kazi za karantini, na udhibiti wa mazao yanayoingizwa nchini au kutolewa nje ya nchi;
- Kuendeleza utafiti wa matumizi ya mbolea ya samadi ya Minjingu inayozalishwa Tanzania Bara. Pindipo matokeo ya utafiti huu yataonesha kwamba mbolea hii inakubaliana na hali ya udongo wa hapa kwetu, tunatarajia kwamba itawapunguzia gharama za uzalishaji wakulima kwa vile mbolea hii ni ya bei nafuu.

**6.4.3.3 Mheshimiwa Spika,** malego ya Kitengo cha Mpunga na Pembejeo ni kama ifuatavyo:

- Kuzalisha ekari 17.5 za mbegu mpya za muhogo katika mashamba mama (mother stock) yaliyomo katika vituo vyta utafiti, na kuzisambaza kwa wakulima wazalishaji mbegu;
- Kuzalisha na kusambaza tani 100 za mbegu ya mpunga, kwa wakulima wa Unguja na Pemba; Mbegu hizi zinatarajiwa kuzalishwa hapa hapa kwa kuwashirikisha wakulima watakaopewa mafunzo maalumu;
- Kusambaza kwa wakulima mbegu mpya ya mahindi aina ya Masaya kutoka Morogoro.
- Kununua matrekta 12 mapya na
- Kununua na kusambaza mbolea tani 1,484 Urea, 1,367 TSP na 63 DAP.

**6.4.3.4 Mheshimiwa Spika**, katiika kuboresha utoaji wa huduma za matrekta, Wizara inaendelea na jithada za kuongeza idadi ya matrekta. Kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara imeandaa mpango maalum wa ununuzi wa matrekta ya ziada lengo ni kuwa na matrekta matano kwa kila wilaya.

**6.4.3.5 Mheshimiwa Spika**, malengo kwa uzalishaji wa miche ya minazi ni kuzalisha miche 15,000 na miche ya matunda 15,000.

#### **6.4.4 MTIZAMO WA SASA**

**6.4.4.1 Mheshimiwa Spika**, mtazamo katika kuendeleza kilimo ni kuongeza uzalishaji wa kilimo cha juu na maweni, na kwa upande wa kilimo cha juu mtazamo wa sasa ni:

- Kuongeza usambazaji wa mbegu bora za mazao ya chakula;
- Kutoa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kutumia mfumo wa skuli za wakulima na
- Kuwaunganisha wakulima wahitimu kutoka skuli za wakulima na kuzifanya kuwa taasisi za wazalishaji na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo.

**6.4.4.2 Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa kilimo cha maweni, mtizamo ni:

- Kuufanya ukanda wa maweni kuwa wa uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo kwa kuandaa taarifa maalumu za kitaalam juu ya aina ya mazao yanayomea vizuri katika ukanda huo na mbinu za kuzalisha mazao hayo;
- Kushajiisha ufugaji mdogo mdogo wa mbuzi na kuku (small stock development) kupitia vikundi vya skuli za wafugaji; na
- Kuendeleza kazi za udhibiti wa wadudu waharibifu na maradhi kwa mazao mbalimbali hasa nzi wa embe na matunda kwa kusambaza mitego kwa wakulima.

**6.4.4.3 Mheshimiwa Spika**, tatozo la mafunza katika matunda ni la kitaifa na la Kikanda, yaani limeenea katika nchi za Afrika ya Mashariki. Hata hivyo, kwa Zanzibar zao la matunda hasa embe lina umuhimu mkubwa wa kibashara, ukilinganisha na nchi nyingine za jirani. Hivyo, pamoja na juhudini zinazochukuliwa na Serikali kupitia Wizara za kudhibiti wadudu hao kwa kutumia mitego, jitihada bado zinahitajika kwa wananchi wote kuheshimu sheria za karantini kwa kuacha kuleta matunda kutoka nje ya nchi bila ya kufuata sheria.

## **6.5 CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI**

**6.5.1 Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba serikali imekipandisha hadhi Chuo cha Kilimo Kizimbani kuwa Idara kamili yenye uwezo wa kujamulia mipango yake ya maendeleo. Hii ikiwa ni kutekeleza Sheria namba tano ya Chuo cha Kilimo Kizimbani. Aidha, Mkurugenzi wa chuo na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo tayari wameshachaguliwa na hatua inayofuata ni kuteuwa wajumbe wa Baraza hilo.

### **6.5.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2008/2009**

**6.5.2.1 Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2008/2009 Chuo kilitekeleza yafuatayo:

- Kilifundisha wanafunzi 57 (17 wanaume na 40 wanawake) ngazi ya cheti, kati yao wanafunzi 50 wanatoka maskuli (pre-service) na wanafunzi saba (7) ni watumishi wa Serikali (in-service). Utekelezaji huo ni sawa na asilimia 162.85 ya lengo. Aidha, lengo hili limefikiwa kutohana na wananchi wengi kukubali kuchangia gharama za mafunzo;
- Kimeimarisha ekari 15 za malisho ya ng'ombe. Hii imetokana na uamuzi wa kuongeza idadi ya ng'ombe wa maziwa kwa ajili ya mafunzo na uzalishaji mitamba.

### **6.5.3 MALENGO KWA MWAKA 2009/2010**

**6.5.3.1 Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2009/2010, chuo kinalenga kukarabati majengo yake, kuajiri wakufunzi, kutoa mafunzo kwa vijana 35 wapya na kuendela na mafunzo kwa wanafunzi 88 (30 wanaume na 58 wanawake) wa mwaka wa pili na kununua vifaa vya maabara na karakana kwa ajili ya mafunzo ya kilimo kwa vitendo. Aidha, kupitia mradi wa usarifu wa Mazao

chuo kitajengewa uwezo zaidi kwa kupatiwa majengo (ofisi na maabara) na vifaa vyake.

## 6.6 IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI

**6.6.1 Mheshimiwa Spika,** Idara inaendelea kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji kama ilivyoainishwa katika Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji kwa lengo la kuongeza uzalishaji, tija na kuimarisha uhakika wa chakula kwa wakulima na Taifa.

### 6.6.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2008/2009

#### 6.6.2.1 Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2008/2009 Idara ilitekeleza yafuatayo:-

- Ekari 450, zimeendelezwa kwa kujenga mitaro mipya, kuchimba visima na kufunga pampu. Kati ya ekari hizo ekari 350 zipo Bumbwisudi na ekari 100 zipo Kibokwa;
- Imehamasisha na kuelimisha wakulima wa kilimo cha umwagiliaji maji 2,500 kutoka Unguja na 1,500 kutoka Pemba juu ya mbinu bora na uhifadhi wa mashamba ya umwagiliaji;
- Iliendeleza mashamba madogo ya umwagiliaji maji ekari 35 (kiwango cha asilimia 60 ya lengo) katika maeneo ya Uzini (ekari 5), Mgenihaji (ekari 20), Matetema (ekari 5) na Kitogani (ekari 5).
- Ilihamasisha umwagiliaji wa kutumia matone (drip irrigation) kwa kaya 40 katika maeneo ya Mpapa (ekari 5), Mzuri (ekari 3.5) na Dunga (ekari 2.5).
- Ilitengeneza miundombinu ya kuvunia maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji katika maeneo ya Kibokwa, Koani na Kiboje kwa Unguja, Weni na Kwapweza kwa Pemba, kwa ukubwa wa hekta 10 kwa kila eneo;
- Ilikarabati majengo ya vituo vya Umwagiliaji maji katika mabonde ya Cheju, Bumbwisudi, Mwera na Tibirinzi kwa asilimia 85;
- Ilipima na kuchora ramani za mabonde ya Masingini na Mlemele yenye ekari 200. Mabonde yote hayo tayari yameandikiwa mradi na kupelekwa kwa wahisani - JAPAN.

#### 6.6.2.2 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008/2009 Idara imetekeliza miradi miwili ya Umwagiliaji Maji ambayo ni Mradi wa Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji na Mradi wa Mpango wa Kilimo cha Kisasa na Maendeleo ya Kilimo Cha

Umwangiliaji Maji Zanzibar. Kwa ujumla miradi hii ina lengo la kuimarisha kilimo cha umwagiliaji nchini kwa kuimarisha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji na kuwajenga uwezo wa kitaaluma wakulima wa umwagiliaji. Maelezo ya utekelezaji wa miradi hii kwa mwaka 2008/2009 yanapatikana katika (**Kiambatisho 9**) na (**Kiambatisho 10**).

### 6.6.3 MALENGO YA MWAKA 2009/2010

**6.6.3.1 Mheshimiwa Spika;** malengo ya Idara kwa mwaka 2009/2010 ni kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji maji kwa kiwango cha ekari 618. Aidha, Idara inalenga kuendeleza mafunzo kwa wakulima na wafanyakazi, kuanzisha mashamba ya mfano na kuwezesha ziara za wakulima. Sambamba na hayo Idara pia itaendelea kutekeleza Mradi wa Mpango wa Kilimo cha Kisasa na Maendeleo ya Kilimo Cha Umwangiliaji Maji Tanzania na kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji.

### 6.6.4 MTIZAMO WA SASA

**6.6.4.1 Mheshimiwa Spika,** mtizamo wa sasa katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji ni:

- Kuendeleza ukarabati wa misingi ya umwagiliaji maji;
- kuongeza taaluma kwa jumuiya za wakulima wa mpunga wa umwagiliaji juu ya uzalishaji bora, mbinu bora za kutumia maji kwa ufanisi na juu ya matunzo ya mashamba ya umwagiliaji;
- kuboresha upatikanaji wa zana na huduma za matrekta, mkazo zaidi utawekwa katika kuendeleza kilimo cha jembe la kukokotwa na ng'ombe na kuongeza upatikanaji wa zana ndogo ndogo;
- Kujenga uwezo wa mafundi wakufunzi, madereva na mafundi katika matumizi ya zana za kilimo;
- Kuongeza uzalishji wa kilimo cha mpunga wa umwagiliaji kwa kutumia skuli za wakulima.

## **6.7 IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO**

- 6.7.1 Mheshimiwa Spika**, mtazamo wa Idara hivi sasa unaelekezwa katika kuongeza ubora wa mifugo kwa lengo la kuongeza tija kwa wazalishaji na kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Katika kufikia lengo hili Idara inaendelea na kukabiliana na changamoto zilizopo na zinazojitokeza ikiwemo maradhi ya miripuko, taaluma duni ya wafugaji, uwekezaji mdogo katika Sekta ya Mifugo na uhaba wa maeneo ya malisho n.k.
- 6.7.2 Mheshimiwa Spika**, miripuko ya maradhi ya mafua ya ndege na mafua ya nguruwe bado yanaendelea kuwa tishio duniani. Hadi sasa jumla ya watu 470 duniani wameambukizwa na 256 wamefariki dunia kutokana na maradhi hayo. Nchi 64 za kiafrika tayari zimethibitishwa kuathirika na maradhi hayo. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya dunia nayo pia inakabiliwa na changamoto ya kujikinga na maradhi hayo. Kutokana na sababu hizo, Wizara inaendelea kutoa taaluma kwa wananchi juu ya athari na njia za kujikinga na maradhi hayo.

### **6.7.3 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2008/2009**

- 6.7.3.1 Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2008/2009 Idara ililenga kusaidia utoaji huduma za tiba, kinga kwa mifugo aina zote, kuendeleza uzalishaji wa kabilia bora za mifugo na kutoa taaluma kwa wafugaji. Utekelezaji halisi wa malengo hayo ni kama ifuatavyo:
- Ilikamilisha mchakato wa ununuzi wa mtambo wa kutengeneza "Liquid nitrogen". Zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mtambo huu tayari zimeshatolewa na kupitishwa na Bodi ya Tenda ya Wizara. Kampuni moja tayari imeshateuliwa kwa ununuzi wa mtambo huo.
  - Ilipandisha ng'ombe 1,841 kwa njia ya sindano;
  - Ilisomesha na kuwapatia vifaa vya kazi wafanyakazi 40 na watoaji huduma za tiba na kinga ya maradhi ya mifugo 90 wanaotoka vijijini (Community Animal Health Workers-CAHWs);
  - Ilinunua na kuwagawia wananchi ng'ombe bora wa maziwa 196 na mbuzi wa maziwa 406;
  - Jumla ya mifugo 103,953 ilipatiwa huduma ya kinga kwa maradhi mbalimbali na mifugo 101,145 walitibiwa ikijumuisha ng'ombe 23,153, mbuzi 20,369 na kuku 57,623;
  - Idara kwa kuwashirikisha vijana vijijini wameendesha zoezi la kuwachanja kuku wa kienyeji dhidi ya maradhi ya Mahepe jumla ya kuku

wa kienyeji 331,291 wamechanjwa kisiwani Unguja (63,928 Kaskazini "A", 37,008 Kaskazini "B", 111,782 Kati, 17,894 Kusini 100,679 Magharibi). Zoezi hili hivi sasa linaendelezwa kisiwani Pemba.

- Ilishajiisha wananchi katika Shehia mbalimbali katika kufichua uingizaji wa mifugo na bidhaa zake kinyume na sheria;
- Iliweka vifaa vipyta vyta kufanya kazi na ilikarabati majengo ya Idara ikiwemo vyumba vyta kufanya upasuaji, ofisi ya daktari na majengo mengine ya Idara;
- Imesafisha asilima 42 ya eneo la Karantini katika kijiji cha Kisakasaka na kurudisha huduma za maji na umeme kwa kutumia jenereta;

#### **6.7.4 MALENGO KWA MWAKA 2009/2010**

##### **6.7.4.1 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010 idara inalenga kutekeza yafuatayo:**

- Kujenga na kukarabati majengo ya Mradi wa Kupandisha ng'ombe kwa sindano (A.I) na Ofisi nyengine ambazo zitatumika kuuhifadhi mtambo wa "Liquid Nitrogen" unaotarajiwa kununuliwa hivi karibuni;
- Kuendeleza huduma za kinga na tiba ya maradhi ya mifugo, kuimarisha kazi za karantini pamoja na kufuutilia mwenendo wa maradhi ya mifugo duniani ili kujiepusha na hatari ya kupata maambukizo ya maradhi ya mifugo kutoka nje ya Zanzibar;
- Kuendeleza mahusiano na mashirikiano na taasisi za kutoa huduma za mifugo zilioko Tanzania Bara na zile za kimataifa;
- Kuendeleza mashamba ya Mifugo ya Serikali kwa nia ya kuwapatia wananchi mifugo bora;
- Kutoa mafuzo kwa wafugaji juu ya ufugaji wa kisasa, udhibiti maradhi ya mifugo na ujenzi wa mitambo ya kutengenezea nishati itokanayo na kinyesi cha mifugo. Mafunzo haya yatatolewa kwa mashirikiana baina ya Idara na Miradi na programu mbalimbali nchini;
- Kuongezeka kwa idadi ya ng'ombe wa maziwa kutoka ng'ombe 9,500 hadi ng'ombe 10,260;
- Kuimarisha huduma za karantini;
- Kuimarisha malisho ya wanyama na kuwapatia wafugaji taaluma ya uzalishaji wa malisho bora.

- 6.7.4.2** **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Idara itatekeleza miradi mitatu ambayo ni Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa, Mradi wa Upandishaji Ng'ombe kwa Sindano na Miradi wa kudhibiti Mafua Makali ya Ndege.
- 6.7.4.3** **Mheshimiwa Spika**, Mradi wa kudhibiti maradhi ya Kichaa cha Mbwa unalenga kutoa chanjo kwa mbwa wanaofugwa na wanaozurura. Mradi unafadhiliwa na Shirika la WSPA kwa Dola za Kimarekani 95,326 na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo itatoa Sh. 25,000,000. Aidha, Mradi wa upandishaji wa ng'ombe kwa sindano utatekelezwa kwa fedha za Serikali na unaombewa Sh. 40, 000,000.
- 6.7.4.4** **Mheshimiwa Spika**, ingawa nchi yetu haikupata kuathiriwa na maradhi ya mafua makali ya ndege, hatuna budi kuendeleza harakati za kudhibiti maradhi hayo yasiingie nchini. Hivi sasa Idara inashirikiana na Mashirika ya AU-IBAR na UNICEF katika kudhibiti maradhi haya kwa kupitia utekelezaji wa Mradi wa kudhibiti mafua makali ya Ndege. Mradi huu utafadhiliwa na Shirika la AU-IBAR ambalo litatoa Dola za Kimarekani 250,000, Shirika la UNICEF ambalo litachangia Dola za Kimarekani 150,000 na Serikalini ambayo itachangia Sh. 50, 000,000.

## 6.7.5 MTIZAMO WA SASA

- 6.7.5.1** **Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza Sekta ya Mifugo, Wizara ina mtizamo ufuatao:
- Kuongeza ubora wa mifugo inayozalishwa. Mkazo zaidi utakuwa katika kutoa mafunzo juu ya lishe bora kwa mifugo ili kupata mifugo bora na kuweza kudhibiti soko la ndani. Lengo ni kuwa na mifugo yenye ubora na viwango vinavokubalika katika soko la utalii;
  - Kusambaza kwa wafugaji huduma za upatikanaji wa mbegu bora za mifugo kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija.
  - Kuendelea na kazi ya udhibiti wa maradhi ya mifugo na wadudu wanaoathiri maendeleo ya sekta ya mifugo.
  - Kuongeza usarifu wa mazao ya mifugo

## **6.8 IDARA YA MAZAO YA BIASHARA, MATUNDA NA MISITU**

**6.8.1 Mheshimiwa Spika,** Idara hii ina majukumu ya kuwashirikisha wananchi kutunza na kuendeleza rasilimali za misitu na wanyama pori, kuhamasisha kilimo cha mazao ya biashara na kusimamia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mazao ya misitu.

### **6.8.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO MWAKA 2008/2009**

**6.8.2.1 Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2008/2009 Idara ilitekeleza yafuatayo:

- Ilisimamia uundwaji wa Kamati za mazingira kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za misitu katika shehia ya Uzi. Kamati hiyo imewajumuisha wakaazi wa Shehia ya Uzi na Ng`ambwa;
- Ilitoa mafunzo kwa wanajamii 273 juu ya uhifadhi wa misitu, ufugaji nyuki na kazi za mikono;
- Ilikarabati majengo ya afisi ya Maruhubi na Kiwengwa;
- Kazi ya upandaji miti kitaifa imefanyika kwa kuhamasisha wananchi kupanda miti. Jumla ya miti 6,000 ya mikangazi na misaji ilipandwa katika vyanzo vya maji vya Masingini tarehe 12/4/2009 ambapo mgeni rasmi alikuwa Mhe, Dk. Amani Abeid Karume- Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye alizindua kampeni hio;
- Iliendeleza utalii wa Hifadhi ya Kiwengwa Pongwe, Msitu wa Hifadhi ya Kimaumbile wa Ngezi Vumawimbi na kuongeza njia za kupita watalii mpaka Wangwani katika Hifadhi ya Taifa ya Jozani na Ghuba ya Chwaka;
- Ilikamilisha rasimu ya mwanzo ya mapitio ya Sera ya Misitu.

### **6.8.3 MALENGO KWA MWAKA 2009/2010**

**6.8.3.1 Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2009/2010 malengo ni kama ifuatavyo:

- Kukamilisha Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali za Misitu ya shehia nane zinazozunguka Msitu wa Hifadhi wa Kiwengwa- Pongwe, shehia nne za Msitu Mkuu na shehia moja ya Ras Kiuyu;
- Kutekeleza Mpango wa muda mrefu wa usimamizi wa Misitu 2009 hadi 2020;
- Kufanya mapitio ya mpango wa usimamizi wa rasilimali za misitu, kwa shehia 10 zilizozunguka Ngezi-Vumawimbi na shehia nane zilizozunguka Hifadhi ya Taifa ya Jozani;

- Kutoa mafunzo kwa kamati 10 za uhifadhi katika wilaya za Unguja na Pemba juu ya kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Rasilimali za Misitu;
- Kukamilisha rasimu ya sera ya misitu;
- Kufanya ukarabati wa afisi na nyumba za wafanyakazi wa vituoni;
- kuimarisha doria katika maeneo ya maliasili za misitu, kutekeleza mpango wa usimamizi wa mikoko na shamba la Makuwe;
- Kuhamasisha jamii kutumia nishati mbadala badala ya kuni na mkaa;
- Kuhamasisha wananchi kuanzisha vitalu, upandaji miti na ufugaji wa nyuki;
- Kutekeleza mpango wa misitu wa muda mrefu wa Idara 2009 - 2020

**6.8.3.2 Mheshimiwa Spika,** pamoja na malengo hayo, Idara pia kwa mwaka 2009/2010 itasimamia Mradi wa Mpango wa Taifa wa Uimarishaji Mikarafuu. Maelezo ya malengo ya utekelezaji wa mradi huu yanapatikana katika **Kiambatisho 11.**

#### 6.8.4 MTIZAMO WA SASA

**6.8.4.1 Mheshimiwa Spika,** mtizamo wa sasa katika kuhifadhi na udhibiti wa rasilimali ni kama ifuatavyo:

- Kuendeleza tafiti za nishati mbadala;
- Kuongeza uzalishaji katika mashamba ya misitu na mbegu;
- Kuwashirikisha wanajamii katika usimamizi wa rasilimali za misitu;
- Kuhamasisha uzalishaji wa asali na nta kwa ubora na viwango vinavyo kubalika katika soko la biashara.

### 6.9 IDARA YA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI

**6.9.1 Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uvubi na Mazao ya Baharini inaendelea na jitihada za kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha matumizi endelevu ya rasilimali za baharini, kuendeleza uvubi mdogo mdogo na kusimamia uvubi katika bahari kuu kwa lengo la kuifanya sekta ya uvubi iwe yenye kulinufaisha Taifa na jamii za wavubi.

## **6.9.2 UTEKELEZAJI MALENGO YA MWAKA 2008/2009**

### **6.9.2.1 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008/2009 Idara ililenga kufanya yafuatayo:**

- Imeendelea na kufaya doria kwa kushirikiana na wanajamii pamoja na kikosi cha KMKM. Jumla ya vyombo vinane vimekamatwa kwa kuvua uvuvi haramu na tayari hatua za kisheria zimechukuliwa;
- Imeanza mchakato wa matayarisho ya ujenzi wa Afisi za Idara;
- Imetoa vifaa kwa wakulima wa mwani vyenye thamani ya Sh. 50,000,000
- Imefanya " Rapid Assessment" kwa maeneo ya Changuu /Bawe na Tumbatu ambayo ni maeneo yaliyopendekezwa kuwa ni ya hifadhi ili kuweza kujua:
  - Maoni na mitazamo ya watu kuhusu wazo hilo la kufanya maeneo hayo kuwa ni ya hifadhi
  - Kuweza kujua vivutio na rasilimali zinazopatikana katika maemeo hayo
  - Kependekenza mipaka ya maeneo hayo ya hifadhi
  - Kuweza kupata mtazamo wa jinsi ya kuyasimamia maeneo hayo ya hifadhi kwa ufanisi zaidi.
- Imeandaa rasimu ya marekebisho ya sheria za uvuvi na hivi sasa imo katika matayarisho ya kupelekwa katika ngazi za juu serikalini;
- Imetoa mafunzo kwa Kamati za Uvuvi juu ya uhifadhi wa rasilimali za baharini na Mazingira yake;
- Imehamasisha uwekezaji katika ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kama vile chaza, kaa nk, lengo ni kupunguza ongezeko la uvuvi baharini.

### **6.9.2.2 Mheshimiwa Spika, Idara ya Uvuvi na Mazao Baharini kwa mwaka 2008/2009 iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa MACEMP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Maelezo ya utekelezaji wa mradi huu yameelezwa katika **Kiambatisho 12.****

### **6.9.3 MALENGO YA MWAKA 2009/2010**

**6.9.3.1 Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2009/2010, Idara itaendelea kuishirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za baharini na Mazingira yake kwa kufanya kazi zifuatazo:

- Kushirikisha jamii katika uhifadhi wa maeneo ya hifadhi ya rasilimali za baharini;
- Kuhamasisha wavuvi wadogo wadogo kujishughulisha na ufugaji wa samaki na mazao mengine ya bahari;
- Kuanzisha utaratibu wa kuzuia nyavu zenyne macho madogo (chini ya inchi mbili) kuingia nchini;
- Kuendeleza kazi za doria katika maeneo ya hifadhi;
- Kuendeleza uwekaji wa matumbawe ya kienyeji katika maeneo ya nje ya hifadhi zetu;
- Itashirikiana na taasisi za Uvuvi Tanzania Bara katika matayarisho ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu.
- Kujenga majengo ya ofisi ya Idara ya Uvuvi Unguja na Pemba pamoja na majengo matatu ya maeneo tengefu (ujenzi utaanza baada ya miezi 3);
- Kufanya utafiti wa mbegu mbadala za kilimo cha mwani mwembamba itakayoweza kuota na kutoa tija bora kwa wakulima wetu;
- Kuhamasisha wakulima wa mwani kuijunga na Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima;
- Kupanua wigo wa maeneo ya uhifadhi pamoja na kuyatangaza kisheria maeneo mapya ya Tumbatu na Mji Mkongwe.
- Kuendelea kusimamia na kutekeleza Mradi wa MACEMP

### **6.9.4 MTIZAMO WA SASA**

**6.9.4.1 Mheshimiwa Spika**, mtizamo wa sasa katika kuendeleza sekta ya uvuvi ni:

- Kuendeleza uvuvi wa vikundi. Lengo ni kuwaelekeza wavuvi waunganishe rasilimali ya nguvukazi ili wawekeze katika uvuvi wa kisasa wenye tija na kulinda mazingira ya bahari;
- Kuendeleza miundombinu ya uhifadhi wa samaki sambamba na taaluma juu ya uhifadhi wa samaki kwa lengo la kuwa na rasilimali zenyne kiwango bora na kupunguza upotevu wa rasilimali hizo.

## 6.10 IDARA YA MAZINGIRA

**6.10.1 Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mazingira ina majukumu ya kushajiisha jamii juu ya uhifadhi wa mazingira ya ardhini, angani na majini; kutoa elimu ya mazingira na miongozo kwa jamii juu ya mbinu bora za kuhifadhi mazingira, pamoja na kuratibu tathmini za kimazingira kwa mipango, programmu na miradi ya maendeleo na vitega uchumi nchini.

### 6.10.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2008/2009

**6.10.2.1 Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2008/2009 utekelezaji wa malengo ya Idara ulikuwa kama ifuatavyo:

- Jumla ya makala sita (6), vipindi vya TV 8 na redio 12 juu ya mabadiliko ya hali ya hewa, misitu, usimamizi na matumizi ya mifuko ya plastiki na hali ya mazingira ya Zanzibar vilitayarishwa na kurushwa hewani kupitia vyombo vya habari vya serikali na vya watu binafsi vya ndani na nje ya nchi;
- Kufanya mapitio ya miradi ya vitega uchumi kwa nia ya kuangalia masuala ya mazingira na kutoa mapendekezao yaliyopelekea kutekelezwa kwa miradi hiyo bila ya kuathiri mazingira na jamii kwa jumla ambapo jumla ya taarifa ya miradi 99 zilifanyiwa mapitio;
- Kushiriki katika makongomano nchini na kutoa mwamko kwa wanajamii juu ya masuala ya mazingira.
- Kurekebisha sheria ndogo ya upigaji marufuku mifuko ya plasitiki ambapo Idara kwa kushirikiana na Manispaa na Kitengo cha Kumlinda Mlaji imeendesha zoezi la ukaguzi katika maduka na watumiaji wa mifuko ya plasitiki. Aidha, semina kwa maafisa wa jeshi la polisi ilifanyika kuweka mikakati ya kusimamia agizo la serikali la upigaji marufuku mifuko ya plasitiki na kuzifahamu sheria zake.
- Idara kupitia mradi wa maji machafu chake chake, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake na Baraza la Mji wa Chake imeweza kukamilisha ‘final design’ ya mradi huo. Aidha, jumla ya makontena manane ya vifaa yamewasilishwa Pemba na kazi za upimaji, uchimbaji na ulazaji mabomba zimekamilika.
- Ilishiriki katika kutoa taaluma kwa wanafunzi wa SUZA, Zanzibar University, Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam, Chuo kikuu cha Norway (Trondom) na wanafunzi wa kimarekani walikuja kwa muda mfupi.

- Idara kwa kushirikiana na bodi ya madawa ilifanya ukaguzi wa bidhaa mbalimbali zilizomaliza muda wake. Jumla ya tani 50 za mchele ulioharibika ambao haufai kuliwa na binaadamu zilipatikana. Kiasi cha tani 40 za unga wa ngano usiofaa kwa matumizi ya binaadamu na tani 33 za tende ziliangamizwa;
- Jumla ya kesi 87 za waliokamatwa na mifuko ya plastiki zilifikishwa Mahakamani na katuni 969 za mifuko zilichomwa moto.

### **6.10.3 MALENGO KWA MWAKA 2009/2010**

#### **6.10.3.1 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Idara inalenga kutekeleza yafuatayo:**

- Kuendeleza kazi za utoaji wa elimu ya mazingira kwa jamii na wawekezaji.
- Kuendeleza kazi za kufanya mapitio ya miradi pamoja na kuratibu tathmini za kimazingira kwa miradi ya maendeleo.
- Kuanzisha viwango vya bidhaa za mitumba.
- Kuendeleza ufuutiliaji wa miradi ya maendeleo.
- Kuendeleza jaa la mfano (Pilot) Wilaya ya Kusini (Kisima kipyा).
- Kuendeleza kufanya tafiti mbalimbali za Bioanuai katika ukanda wa maweni.
- Kuendeleza kazi za uhifadhi wa kasa pamoja na kufanya utafiti juu ya mazingira ya maisha ya wanyama hao.
- Kusimamia upigaji marufuku uingizwaji na matumizi ya mifuko ya plasitiki.
- Kuandaa nyenzo za kufundishia /kuhamasisha elimu ya mazingira.
- Kukamilisha mapitio ya sera na sheria ya mazingira.
- Kutayarisha miongozo ya tathmini za athari za kimazingira.
- Kutekeleza kazi za mpango wenye uwiyano wa maeneo ya pwani.

#### **6.10.3.2 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Idara ilitekeleza miradi miwili ambayo ni mradi wa matumizi Endelevu ya Ardhi na Mazingira (SMOLE) na Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani (MACEMP).**

**6.10.3.3 Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2009/2010 pamoja na malengo hayo, Idara pia inategemea kutekeleza programu moja ya Usimamizi wa Mazingira kwa Maendeleo Endelevu. Programu ina lengo la kuwajengea uwezo jamii hasa inayotumia rasilimali za baharini na ukanda wa pwani. Aidha, programu itatekelezwa katika mfumo wa miradi midogo midogo mitatu ambayo ni:

- Mradi wa Kudhibiti Maji Machafu;
- Mradi wa Changamoto za Milenia Tanzania (MCA-T);
- Programu ya Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani kwa nchi za Magharibi ya Bahari ya Hindi (ReCoMaP).

#### **Mradi wa Kudhibiti Maji Machafu**

**6.10.3.4 Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa katika Shehia ya Msingini-Mtoni, katika Wilaya ya Chake Chake Pemba na una lengo la kurekebisha mfumo wa maji machafu katika shehia hiyo. Marekebisho hayo yatahusisha kutenganisha maji machafu kutoka kwenye makaro na yale ya mvua kabla ya kuyamwaga baharini. Aidha, mradi pia unalenga kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kudumisha usafi katika maeneo yanayowazunguka ili kupunguza mripuko wa maradhi. Mradi unafadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Mazingira (UNEP) ambalo litatoa Euro 150,000, TASAF ambayo itatoa Sh. 60,000,000 na Serikali ambayo itachangia Sh. 15,000,000.

#### **Mradi wa Changamoto za Milenia Tanzania (MCA-T)**

**6.10.3.5 Mheshimiwa Spika**, Idara ya mazingira itashiriki katika kutekeleza Mradi wa Changamoto za Milenia Tanzania kwa kuweka njia nyengine mpya ya umeme kutoka Tanzania Bara (Dar es Salaam-Ubungo) hadi Zanzibar (Mtoni) kupitia chini ya bahari kati ya Ras Kilomoni na Fumba. Jukumu la Idara katika mradi huu ni kusimamia tathmini za kimazingira, kuendesha zoezi la ufuatilaji wa masuala ya kimazingira pamoja na kuweka miongozo ya kufuatwa wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo. Katika kutekeleza kazi hizo Idara itapata Dola za Kimarekani 96,350 kutoka katika akaunti ya Millenia na Serikali itachangia Sh. 15,000,000.

**Programu ya Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani kwa nchi za Magharibi ya Bahari ya Hindi (ReCoMaP).**

**6.10.3.6 Mheshimiwa Spika**, Programu hii ni ya kimataifa na inatekelezwa na nchi saba za Afrika ambazo ni Kenya, Msumbiji, Mauritius, Seychelles, Madagasca, Tanzania na Somalia. Mradi huu una lengo la kutoa elimu kwa jamii ya ukanda wa pwani juu ya kuhifadhi rasilimali za ukanda huo. Miongoni mwa kazi zinazotekelizwa na mradi huu ni pamoja na upandaji wa mikoko, ufugaji wa samaki, kaa, kombe na nyuki, usafi wa mazingira ya fukwe, kuhamasisha wanafunzi na wakulima wa mwani na utunzaji wa mazingira. Katika kufanikisha kazi hizi Idara inatarajia kupata kiasi cha Euro 20,000 kutoka Jumuia ya Nchi za Ulaya na inaombewa jumla ya Sh. 10,000,000 kutoka Serikalini.

#### **6.10.4 MTIZAMO WA SASA**

**6.10.4.1 Mheshimiwa Spika**, Mtazamo wa sasa wa Idara ni kuongeza ushiriki wa wanajamii katika uhifadhi wa mazingira hasa katika ukanda wa pwani na katika maeneo yaliyotambuliwa kuwa yamo katika hatari ya uharibifu.

### **6.11 IDARA YA VYAMA VYA USHIRIKA**

**6.11.1 Mheshimiwa Spika**, suala la kuendeleza vyama vya ushirika kwa wazalishaji wadogo wadogo linapewa kipaumbele cha kipekee na Wizara yangu kwa vile uzowefu unaonesha kwamba vyama hivi vina nafasi kubwa katika kuweka mazingira mazuri ya kuongeza uzalishaji, kuweka maslahi mazuri ya wazalishaji na kuongeza tija. Aidha, katika utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyo chini ya Wizara, uanzishwaji wa vyama vya ushirika unakwenda sambamba na utoaji wa huduma za kitaaluma kwa lengo la kuimarisha umoja kwa wazalishaji wadogo wadogo.

#### **6.11.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2008/2009**

**6.11.2.1 Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza kazi za ushirika, Idara kwa mwaka 2008/2009 ilitekeleza yafuatayo:

- Ilisajili vyama vipyta vya ushirika 327 (180 Unguja na 147 Pemba) kati ya hivyo 74 vya Akiba na Mikopo (SACCOS) na 253 vya uzalishaji;

- Ilikamilisha rasimu ya kwanza ya Sera ya Ushirika kwa mashirikiano na Shirika la Kazi Duniani (ILO) na kuiwasilisha kwa wadau mbalimbali ili kupata maoni yao;
- Ilitoa mafunzo kwa wanaushirika juu ya uanzishwaji na uongozi wa vyama vya Akiba na Mikopo vijijini. Mafunzo hayo yaliwashirikisha wanaushirika 18,020 (Unguja 10,812 na 7,208 Pemba);
- Ilitoa mafunzo kwa mabwana na mabibi shamba 270 juu ya SACCOS ili nao waipeleke elimu hiyo kwa wazalishaji;
- Ilikagua vyama vya ushirikia 38 Unguja na Pemba.

### **6.11.3 MALENGO YA MWAKA 2009/2010**

#### **6.11.3.1 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010 Idara inalenga kufanya yafuatayo:**

- Kuhamasisha wananchi kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo na vikundi vya miradi ya uzalishaji;
- Kukamilisha utayarishaji wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika;
- Kuendeleza na kujenga uwezo kwa vyama vya ushirika 120 katika Wilaya za Unguja na Pemba kwa kuwapatia mafunzo na huduma mbalimbali za kitaalamu;
- Kujenga uwezo wa Idara kwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi na kuwapatia vitendea kazi;
- Kuendeleza mashirikiano na taasisi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali (NGO's);
- Kukagua vyama vya Ushirika 150 (Unguja 90 na Pemba 60).

### **6.11.4 MTIZAMO WA SASA**

#### **6.11.4.1 Mheshimiwa Spika, mtizamo wa wizara katika kundeleza ushirika nchini ni:**

- Kuimarisha vyama vya ushirika. Mtazamo ni kuwa na vyama imara vya kitaifa vya mazao (commodity based associations) ambavyo vitakuwa vinasimamia suala la masoko na bei ya mazao hayo;
- Kuendeleza vyama vya ushirika vya akiba na mikopo (SACCOS). Mtazamo ni kuwa na SACCOS imara na endelevu zitakazotoa mikopo kwa wajasiriamali na wazalishaji wadogo wadogo.

## **6.12 KARAKANA YA MATREKTA**

**6.12.1 Mheshimiwa Spika,** Karakana ya Matrekta inatoa huduma za kiufundi ikiwa ni pamoja na kutengeneza matrekta, gari pamoja na kufanya kazi za uchongaji na uchomaji.

### **6.12.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2008/2009**

**6.12.2.1 Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi kilichomalizikia Aprili 2009 Karakana imetekeleza malengo yafuatayo:

- Imetengeneza na kuyahudumia matrekta 17, yakiwa ni pamoja na 12 mapya kati ya hayo, 13 Unguja na manne Pemba sawa na asilimia mia moja ya lengo;
- Imekodisha trekta moja kwa kazi za ukulima wa mpunga ikiwa ni sawa ya asimia 50 ya lengo;
- Iliendelea kutoa huduma za uchongaji na uchomaji;
- Mafunzo ya amali (Vocational training) yaliendelea kutolewa kwa vijana kutoka taasisi za serikali na watu binafsi. Wanafunzi wapya 25 waliandikishwa;
- Karakana ilikusanya jumla ya Sh. **17,860,000** sawa na asilimia 56.39 ya lengo na kutumia jumla ya Sh. **17,321,030** ikiwa ni sawa na asilimia 58.67 ya lengo. Matarajio hadi kufikia Juni 2009, makusanyo ya fedha yatafikia Sh. **24,338,280** ambayo ni sawa na asilimia 76.85 na matumizi yatafikia Sh. **24,104,170** sawa na asilimia 81.64 ya makadirio.

### **6.12.3 MALENGO YA MWAKA 2009/2010**

**6.12.3.1 Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2009/2010, Karakana imelenga kutekeleza malengo yafuatayo:

- Kutengeneza na kuyahudumia matrekta 33 yakiwemo matrekta 12 mapya.
- Kukodisha matrekta mawili kwa kazi za ukulima.
- Kutoa huduma za uchongaji na uchomaji
- Kuendelea kutoa mafunzo ya amali (Vocational Training) kwa vijana kutoka taasisi za Serikali na watu binafsi.
- Kukusanya jumla ya Sh. **50,213,500** na kutumia jumla ya Sh. **47,595,000**

## **7.0 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2008/2009**

### **7.1 Makusanyo ya Mapato 2008/2009**

**7.1.1 Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2008/2009, Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya Sh. **696,702,000** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia April 2009, Wizara imekusanya jumla ya Sh. **1,098,930,556** sawa na asilimia **157.73** ya makadirio. Hadi kufikia Juni, 2009, Wizara inakadiria kukusanya jumla ya Sh. 50,000,000 na kufanya makusanyo yote kwa ujumla kufikia Sh. 1,148,930,556 Hii ni sawa na asilimia 165 ya lengo (**Kiambatisho 13**).

### **7.2 Matumizi ya Fedha 2008/2009**

**7.2.1 Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Wizara ya Kilimo Mifugo na Mazingira iliidhinishiwa jumla ya Sh. **26,335,997,000** ambapo Sh. **6,447,274,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, na Sh. **19,888,723,000** kwa kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, Sh. **1,300,000,000** zilikuwa mchango wa Serikali na Sh. **18,588,723,000** zilikuwa mchango wa wahisani.

**7.2.2 Mheshimiwa Spika**, kuanzia Julai 2008 hadi April 2009, Wizara imepata jumla ya Sh. **11,680,754,041.60** sawa na asilimia **44.34** ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa. Kwa kazi za kawaida hadi kufikia April 2009, Wizara imepata Sh. **4,642,811,500** ambayo ni sawa na asilimia **72.01** ya fedha zilizoombw. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo hadi kufikia April, 2009 jumla ya Sh. **702,823,320.30** ikiwa ni sawa na asilimia **54.06** ya fedha zilizoombw ikiwa ni mchango wa Serikali (**Kiambatisho 14**) na jumla ya Sh. **6,335,119,221.30** zilizopatikana ikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo, **sawa na asilimia 34** ya fedha zilizoahidiwa.

## **8.0 MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA 2009/2010**

**8.1 Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira inakadiriwa kukusanya mapato ya Sh. **1,429,900,000**. Aidha, Wizara inatarajia kutumia Sh. **26,559,663,000** kwa kazi za kawaida na kutekeleza miradi 17 ya maendeleo. Kwa kazi za kawaida wizara imepangiwa kutumia Sh. 6,803,300,000 na kwa kazi za maendeleo Sh. 19,756,363,000 zitatumika (ikiwa Sh. 1,650,000,000 ni mchango wa SMZ na Sh. 18,106,363,000 ni mchango wa Washirika wa Maendeleo.

## **9.0 SHUKRANI**

- 9.1** **Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuzishukuru Serikali za nchi zifuatazo – Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Egypt, Afrika ya Kusini, China, Jamhuri ya Korea, Japan, India, Iran, Israel, Finland, Uholanzi, Austria, Australia, Cuba, USA, UK. Aidha, napenda kuyashukuru mashirika mbalimbali ya maendeleo yakiwemo FAO, Benki ya Dunia, IFAD, Benki ya Maendeleo ya Afrika, KOICA, JICA, USAID, UNDP, WSPA, WFP, WWF, IAEA, FFI, WCS ,MCC, UNEP, IOTC, ACTION AID, GLOBAL FUND, IDA, IOTC, UNEP, UNICEF, DANIDA, MCC, Chuo Kikuu cha Turku (Finland). Pia tunazishukuru Jumuiya za EAC, EU, SADC, AU FARM AFRICA Rockefeller Foundation. Aidha, tunazishukuru Wizara za SMZ na taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali zinazosaidia kuleta maendeleo ya Sekta ya Kilimo.
- 9.2** **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii, kuwashukuru wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara Unguja na Pemba kwa kazi zao nzuri na zenye ufanisi wa hali ya juu. Vilevile, nawapongeza Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, wakulima, wafugaji, wavuvi, wanamazingira na wanaushirika wote kwa kazi zao nzuri za kuleta maendeleo katika Sekta ya Kilimo. Aidha, navipongeza vyombo vyote vya habari kwa utoaji wa habari za Sekta ya Kilimo.
- 9.3** **Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Serikali, Wizara yangu inatoa shukurani za pekee kwa FAO kwa msaada wa mbegu na mbolea waliotupatia ambao umewanufaisha wakulima walio wengi na Taifa kwa ujumla. Aidha, napenda kuchukuwa fursa hii kuzishukuru Taasisi zisizo za kiserikali hususan PIRO iliyopo Pemba na ZAFFIDE iliyopo Unguja kwa kufanikisha zoezi la usambazaji wa msaada huo na kuwafikia walengwa kwa wakati.
- 9.4** **Mheshimiwa Spika**, taasisi hizi ni za kupigiwa mfano kwani zimekua karibu sana na Wizara katika utoaji wa huduma mbalimbali za kilimo. Naomba taasisi nyengine za aina kama hii ziige mfano wa taasisi hizi. Aidha, napenda pia kuishukuru Jumuiya ya Wazalishaji, Wenye Viwanda na Wakulima (ZNCIA) kwa mashirikiano ya karibu na Wizira yangu.

## **10.0 HITIMISHO**

- 10.1 Mheshimiwa Spika**, nawaomba waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee na kuijadili bajeti ya Wizara yangu na watupe ushauri na maoni yao juu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa manufaa ya wakulima na Taifa kwa ujumla. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. **26,559,663,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa mwaka 2009/2010. Kati ya fedha hizo, Sh. **6,447,274,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Sh. **19,888,723,000** ni kwa ajili ya matumizi kwa kazi za miradi ya maendeleo.

## **10.2 MHESHIMIWA SPIKA, NAOMBA KUTOA HOJA**

**MHE. BURHAN SAADAT HAJI (MBM)**  
**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA**  
**ZANZIBAR**

**KIAMBATISHO Na. 1. TAKWIMU ZA UZALISHAJI WA MAZAO  
KWA TANI MWAKA 2008/2009**

Mwaka	2004	2005	2006	2007	2008	JUMLA
<b>Mazao</b>						
Mahindi	2,515	1,419	3,927	1,931	1,920	11,712
Mtama	145	459	409	794	610	2417.65
Mpunga	20,405	15,935	24,730	20,038	20,857	101,965
Muhogo	166,106	102,886	190,266	187,213	153,050	799,522
Ndizi	37,998	22,984	88,438	93,641	100,873	343,934
Viazi vitamu	36,018	13,211	63,949	45,620	55,294	214,093
Viazi Vikuu	3,691	2,394	5,100	8,192	3,516	22,893
Majimbi	3,227	7,542	8,408	4,191	8,459	31,827
Njugu Nyasa	105	302	1,800	76	465	2,748

**KIAMBATISHO NA. 2 MAFUNZO KWA WAFANYAKAZI**

<b>IDARA</b>	<b>AINA YA MASOMO</b>		<b>JUMLA</b>
	MAFUNZO YA MUDA MREFU	MAFUNZO YA MUDA MFUPI	
MAZAO YA BIASHARA MATUND NA MISITU	2	21	23
KAMISHENI YA KILIMO, U/E/WAKULIMA	17	16	33
MAENDELEO YA MIFUGO	17	9	26
UMWANGILIAJI MAJI	8	25	33
MAZINGIRA	13	28	41
UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI	12	9	21
SERA NA MIPANGO	3	20	23
VYAMA VYA USHIRIKA	-	2	2
<b>JUMLA</b>	<b>72</b>	<b>130</b>	<b>202</b>

### KIAMBATISHO Na. 3. PROGRAMU YA KUENDELEZA HUDUMA ZA KILIMO (ASSP)

#### Maelezo Mafupi ya Mradi:

Programu hii imeanza Januari 2007 ikiwa na madhumuni ya kuwawezesha wakulima kupata na kutumia utaalamu na teknolojia za kilimo ambazo zitaongeza uzalishaji na kumuongezea mkulima kipato na uhakika wa chakula. Programu inalenga kujenga mashirikiano kati ya taasisi za umma na za watu binafsi katika kutoa huduma bora kwa wakulima. Aidha Programu itaimarisha mfumo wa habari za masoko, na kuongeza uwezo wa upatikanaji wa pembejeo. Programu inatekelezwa katika Wilaya tisa za Unguja na Pemba ikianzia na shehia kumi kila Wilaya.

**Gharama:** USD 5.9 millioni, **Wachangiaji:** SMZ 22%, IFAD 77.1 %, Walengwa 0.7%

**Lengo Kuu:** Kuinua hali ya maisha ya wakulima kwa kuongeza uzalishaji wenye tija, kuongeza kipato, uhakika wa chakula na kupunguza umaskini

#### Bajeti ya mwaka 2008/2009:

Jumla ya Sh. 2,818,916,006, IFAD Sh. 2,171,851,384, SMZ TSh.s. 185,000,000, na Walengwa Sh. 18,929570.

#### Utekelezaji 2008/2009:

1. Upembusi shirikishi umefanyika katika shehia 18 (10 Unguja na 8 Pemba)
2. Vikundi 216 vya skuli za wakulima viliendelea kupewa elimu na 72 vimeanzishwa.
3. Programu imeendelea kutoa Mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 15 katika ngazi zifuatazo: shahada ya juu 4, shahada 6, stashahada 4, astashahada mmoja.  
Mafunzo mafupi yametolewa kwa wafanyakazi 20 (14 wanaume 6 wanawake) kutoka idara ya ya Vyama vya Ushirika juu ya mfumo wa SACCOS, wafanyakazi watatu wa program walipatiwa mafunzo juu ya uendeshaji wa mikopo Arusha,
4. Ziara za kimafunzo zilifanyika Chake Chake ambapo wafugaji wa Mnarani (Kutoka Upenja) walitembelea wenzao wa skuli ya Tekeleza ya Mavungwa Chake Chake na wanakikundi hao wa Skuli ya Tekeleza walipatiwa ziara ya kwenda Mbeya kwa wafugaji wenzao ili kujifunza na kubadilishana mawazo juu ya ufugaji kuku wa kienyeji. Skuli za wakulima 63 Unguja na Pemba walitembeleana kwa kujifunza na kubadilishana mawazo.
5. Programu imeendelea kusaidia shughuli za utafiti katika upandishaji miembe Makunduchi, Donge na Kinduni, utafiti wa rutuba katika maeneo mbalimbali, utafiti wa uzalishaji mbegu za mtama, mahindi, ufuta, embe na muhogo

**Bajeti ya mwaka 2009/2010:** Programu inatarajia kutumia jumla ya Sh. 1,591,502,195, SMZ Sh. 360,000,000, IFAD Sh. 1,220,361,680, walengwa Sh. 11,140,515

#### Malengo ya Mwaka 2009/2010:

1. Kuendelea kuvipatia elimu vikundi vya skuli za wakulima
2. Kuandaa ziara za kimafunzo ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara
3. Kuimarisha shughuli za utafiti na elimu kwa wakulima
4. Kuandaa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi
5. Kukarabati ofisi za Programu Unguja na Pemba.

## KIAMBATISHO Na. 4 PROGRAMU YA KUENDELEZA HUDUMA ZA-MIFUGO (ASDP- L)

### Maelezo Mafupi ya Mradi:

Programu hii imeanza Januari 2007 ikiwa na madhumuni ya kuwawezesha na kuwaendeleza wafugaji masikini ili kuinua hali yao ya kipato na kuwaondoshea umaskini. Programu inatekelezwa katika wilaya tisa za Unguja na Pemba ikianzia na Shehia kumi kila wilaya.

**Gharama za mradi:** USD 3.76 millioni, Wachangiaji: SMZ (6.1%), IFAD (93 %,) WALENGWA (0.9%)

**Lengo Kuu:** Kupunguza umaskini, kuongeza uhakika wa chakula, kuongeza kipato cha watu masikini wanaotegemea mifugo katika maisha yao.

### Bajeti ya mwaka 2008/2009:

Jumla Sh.1,896,153,000, IFAD Sh. 1,743,029,373, SMS Sh. 55,000,000, walengwa Sh.16,551,078

### Utekelezaji 2008/2009

1. Utafiti wa matatizo ya wafugaji haukufanyika kwa sababu wafugaji wenyewe hawakuibua matatizo
2. Kutambua huduma zinazohitajika ili kuwawezesha wafugaji kuongeza uzalishaji na kuzalisha kibiashara na kufanya utafiti wa mfumo wa uzalishaji wa mifugo (imo katika utaratibu wa manunuzi (procurement procedures)
3. Matayarisho yameanza ya ukarabati wa vituo na maabara za mifugo
4. Mafunzo ya watoa huduma za msingi za mifugo kutoka Shehia mbalimbali Unguja na Pemba yamefanyika kwa watoa huduma 90 (66 wanaume na 24 wanawake)

**Bajeti ya mwaka 2009/2010:** Jumla Sh. 1,613,970,657, IFAD Sh. 1,499,444,939; SMZ Sh. 100,000,000, na Walengwa Sh. 14,525,736

### Malengo ya mwaka 2009/2010

1. Kufanya utafiti wa mfumo wa uzalishaji wa mifugo (kuku, ng'ombe na wanyama wadogo wadogo
2. Kufanya ukarabati wa vituo na maabara za mifugo
3. Kutambua huduma zinazohitajika iii kuwawezesha wafugaji kuongeza uzalishaji na kuzalisha kibiashara

## KIAMBATISHO Na. 5 PROGRAMU YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE

### Maelezo mafupi ya Programu:

Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe imeandaliwa sambamba na Sera ili kuwa na Mpango unaotosheleza na unaohusisha sekta na wadau wote katika ngazi za utekelezaji wa malengo ya kukabiliana na kutokuwa na Uhakika wa Chakula na Lishe kama yalivyoelekezwa na MKUZA na Sera ya Taifa ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Programu hii imebuniwa kwa kuzingatia haja ya kusaidiana na juhudzi zilizopo za kupunguza umasikini na kutokuwa na Uhakika wa Chakula na hivyo inaelekeza kazi na hatua muhimu kwa sekta ya Kilimo na sekta nyenginezo katika kutatua matatizo ya kutokuwa na Uhakika wa Chakula na Utapiamlo

**Gharama:** USD 15 milioni katika awamu ya miaka mitano ya mwanzo

**Wachangiaji:** SMZ, FAO, UNICEF, WFP, UNDP na Washirika wengine wa Maendeleo

### Lengo Kuu:

Lengo kuu la Programu ni kuchangia katika hatua za kitaifa za kupunguza umasikini na njaa, kukabiliana na hali ya kutokuwa na uhakika wa chakula na lishe katika ngazi za Taifa, Jamii na Kaya na kushajiisha ushirikiano wa jamii katika hatua za kujiongezea kipato, kuondoa njaa na kufikia hali ya kila mtu ya kuwa na haki ya kula na kushiba

### Gharama mwaka 2008/2009

Programu iliombewa Sh. 64,000,000 kutoka SMZ na inatarajia kutumia USD 104,000 kutoka FAO kuititia UN- Joint Programme 5

### UTEKELEZAJI WA MALENGO 2008/09.

- Uzinduzi rasmi wa Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe ulifanyika tarehe 16 Oktoba, 2008 sambamba na sherehe za maadhisho ya siku ya chakula duniani.
- Matengenezo ya ofisi ya Uratibu wa kazi pamoja na kuweka vifaa vya kazi na fanicha.
- Kamati ya kitaifa ya Tathmini na Ufuatiliaji imeundwa na kuwezeshwa. Matayarisho ya mfumo wa tathmini na ufuatiliaji (Zanzibar Food Security and Evaluation Monitoring and Evaluation Framework). Rasimu tangulizi ya Mfumo imekamilika na kazi za mashauriano na wadau mbalimbali inaendelea.
- Mfumo wa utoaji taarifa za upatikanaji na matumizi ya chakula kitaifa (Zanzibar Food Balance Sheet and Supply Utilization Account) umeandaliwa. Kamati ya kitaifa ya kusimamia kazi hii imeundwa na kupatiwa mafunzo, ofisi na vifaa vya kazi.. Kazi ya kukusanya na kurekebisha takwimu zinazohusika na utoaji taarifa za Food Balance Sheet kwa kipindi cha mwaka 2000 hadi 2007 imekamilika.
- Kamati ya kitaifa ya matayarisho ya Sera na Mkakati wa masoko ya bidhaa za kilimo imeundwa na kuwezeshwa. Kazi za matayarisho ya Sera na Mkakati wa masoko ya kilimo (Zanzibar Agricultural Marketing Policy and Strategy) inaendelea. Rasimu tangulizi imekamilika na mpango wa mashauriano na wadau mbalimbali umeandaliwa.
- Kazi ya matayarisho ya Rasimu ya Sheria itayopelekea kuundwa na kufanyakazi kwa Divisheni ya Uhakika wa Chakula na Lishe ndani ya Wizara ya Kilimo (Food Security Bill) imeanza kwa kuunda timu ya wataalamu wakiwemo maofisa wa sheria wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
- Programu imeratibu na kuwezesha mkakati wa uzalishaji mbegu bora za mpunga kuititia Skuli za Wakulima zinazoendeshwa kwa mashirikiano kati ya Programu ya Huduma za Kilimo, kitengo cha uzalishaji mbegu na idara ya umwagiliaji. Jumla ya skuli 15 za

Wakulima wa Mbegu ya mpunga zimeanzishwa katika bonde la Mtwango, Cheju na Kibokwa ambapo jumla ya wakulima 375 wameshirikishwa. Lengo ni kuzalisha tani 300 za mbegu bora ya mpunga kwa msimu wa kilimo wa 2009/2010. Aidha Programu imezisaidia skuli 5 za wakulima zilizohitimu katika kuendeleza ufugaji wa kuku wa kienyeji na kilimo cha migomba ambapo jumla ya wakulima wahitim100 wamefaidika

Gharama mwaka 2009/2010: Sh. 160,000,000 kutoka SMZ na USD 150,000 kutoka FAO kupitia UN- Joint Programme 5 na USD 200,000 kutoka Serikali ya Ujerumani

### **Malengo ya mwaka 2009/2010**

- Kusimamia shughuli za uratibu wa programu na kuanzisha ofisi ndogo ya uratibu Pemba
- Kuweka na kuwezesha muundo wa usimamizi katika ngazi ya Taifa, Wilaya na Jamii
- Kukamilisha rasimu ya sheria itayopelekea kuundwa na kufanyakazi kwa Divisheni ya Uhakika wa Chakula na Lishe ndani ya Wizara ya Kilimo ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe
- Kukamilisha matayarisho ya sera ya masoko ya kilimo ikiwa ni pamoja na mpango wa utekelezaji wa sera hyo
- Kuimarisha uzalishaji wa chakula ndani ya nchi kwa kuwezesha ongezeko la tija kupitia mkakati wa uzalishaji mbegu bora za mpunga.
- Kuchochea ongezeko la uzalishaji na tija kwa kuwezesha skuli za wakulima na mashamba ya mfano ya uzalishaji wa mpunga na mboga mboga, uimarishaji wa bustani za majumbani na uzalishaji wa mifugo.
- Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu kwa ajili ya tathmini na ufuutiliaji wa kazi za uhakika wa chakula na lishe kwa:
- Kuweka mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za kila siku za mazao na mifugo
- Kuweka mfumo wa ukusanyaji wa taarifa kila siku za Wizara ya Biashara zinazohusu biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara
- Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji taarifa za masoko makuu na masoko ya wilaya
- Kuandaa na kuchapisha matokeo ya kazi za Tathmini na Ufuutiliaji ikiwemo:
  - Ripoti ya mwaka ya mfumo wa upatikanaji na matumizi ya chakula (Food Balance)
- Sheet Report)
  - Jarida la chakula na lishe kwa mwaka
  - Kuandaa dondo za sera (FSN Policy briefs) kwa kila robo mwaka
  - Taarifa za hali halisi ya chakula na lishe kwa wilaya mbili teule.
- Kusambaza matokeo ya kazi za ufuutiliaji kwa kupitia vyombo vy ya habari
- Kuhamasisha uelewa wa Sera na Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe katika ngazi za Taifa, Wilaya na Jamii.
- Kujenga uwezo wa Wilaya na Jamii kupanga mipango ya maendeleo inayozingatia suala la Uhakika wa Chakula na Lishe.

## KIAMBATISHO Na. 6 MRADI WA USARIFU WA MAZAO YA KILIMO

### Maelezo mafupi ya mradi:

Mradi wa Usarifu wa mazao Kilimo ni mradi wa miaka mitatu ambao ulioanza mwaka 2008/2009 kwa kazi za maandalizi ya ujenzi pamoja na vifaa. Mradi unatarajiwa kumalizika Juni 2011. Madhumuni ya mradi ni kujenga kituo cha mafunzo usarifu wa mazao ya kilimo kwa wakulima na wajasiriamali wadogo wadogo, kwa lengo la kutoa taaluma ya usarifu wa mazao pamoja na taaluma ya ujasiriamali.

**Muda wa Mradi:** Miaka mitatu, (Julai 2008/Juni 2011)

**Gharama/Wachangiaji.** KOICA: US \$ 2.300 milioni 2. SMZ US \$ 0.400 milioni

**Lengo kuu:** Kujenga uwezo wa wakulima juu ya usarifu wa mazao na ujasiriamali pamoja na kutoa huduma za udhibiti wa ubora kwa bidhaa zinazozalishwa kwa lengo la kuongeza ajira na kipato kwa wazalishaji.

**Gharama kwa mwaka 2008/2009:** Sh 25,000,000/= SMZ

### Malengo ya mwaka 2008/2009:

- Kugharamia kazi zote za maandalizi ya uanzishwaji wa mradi ikiwa ni pamoja na : Kusafisha eneo la ujenzi wa kituo
- Kufanya uchambuzi wa udongo katika eneo la ujenzi
- Kufanya matengenezo ya kisima ambacho kinatarajiwa kupeleka maji katika kituo pamoja na kufanya uchunguzi wa maji yanayotarajiwa kutumika kituoni.
- Kufanya matengenezo ya barabara ya kuingilia na kutokea katika eneo la ujenzi
- Kuweka uzio wa eneo la ujenzi wa kituo.
- Kununua vifaa kwa ajili ya afisi ya muda ya mradi
- Kutafuta mtaalamu wa kuanisha aina, idadi na uwezo wa vifaa vya kusarifia pamoja na vifaa vya maabara vitakavyo hitajika.

### • Utekelezaji 2008/2009:

- Kazi ya uchambuzi wa udongo katika eneo la ujenzi imekamilika
- Afisi ya muda ya mradi imefanyiwa matengenezo na kuekewa vifaa vyote muhimu.
- Kazi ya kuanisha aina, idadi na uwezo wa vifaa vya kusarifia pamoja na vifaa vya maabara vitakavyohitajika imekamilika.

**Gharama kwa mwaka 2009/2010: US\$ 2.3 milioni – KOICA na SMZ Sh. 170,000,000**

### Malengo ya mwaka 2009/2010:

- Kugharamia kazi zote za maandalizi ya uanzishwaji wa mradi zilizo salia ikiwa ni pamoja na : kusafisha eneo la ujenzi wa kituo
- Kufanya matengenezo ya kisima ambacho kinatarajiwa kupeleka maji katika kituo pamoja na kufanya uchunguzi wa maji yanayotarajiwa kutumika kituoni.
- Kufanya matengenezo ya barabara ya kuingilia na kutokea katika eneo la ujenzi
- Kuweka uzio wa eneo la ujenzi wa kituo.
- Kununua vifaa zaidi kwa ajili ya afisi ya mradi
- Kuweka miundombinu ya maji na umeme katika eneo la ujenzi

- Kutoa mafunzo ya usarifu kwa maafisa wa mradi nchini Korea ya Kusini
- Kuandaa michoro/ ramani ya majengo na kituo cha usarifu wa mazao pamoja na maabara ya uchunguzi wa vyakula
- Kujenga kituo cha usarifu wa mazao
- Kununua na kufunga vifaa vya usarifu wa mazao pamoja na vifaa vya maabara
- Kutoa mafunzo kwa maafisa mradi juu ya namna kuvitumia na kuvitunza vifaa hivyo,
- Kutoa mafunzo ya usarifu wa mazao na ujasiri amali kwa wakulima na wazalishaji wengine.
- Kutoa huduma za udhibiti wa ubora (quality control and assurance services) kwa mazao yaliosarifiwa.

## KIAMBATISHO Na. 7 PROGRAMU NDOGO YA KUHAMASISHA NA KUTOA MAFUNZO YA UKIMWI

### Maelezo mafupi ya mradi:

Programu ndogo ya Elimu ya UKIMWI Katika Sehemu za Kazi  
Mradi huu umeanza tokea mwaka 2005/2006. Programu ina madhumuni ya kutoa taaluma sahihi ya UKIMWI kwa wafanyakazi wa Wizara pamoja wadau wa Sekta ya Kilimo..

**Muda wa Programu:** hadi pale itakapoonekana haja ya kuwepo kwake haipo tena.

**Lengo kuu:** kutoa elumu sahihi ya VVU na UKIMWI kwa wafanyakazi, wakulima, wavuvi, wafugaji pamoja na wanaushirika kwa lengo la kupunguza/kuzuia maambukizi ya VVU mionganoni mwa wadau wa Sekta ya Kilimo.

**Gharama kwa mwaka 2008/2009:** Sh. 15,000,000/= SMZ

### Utekelezaji 2008/2009:

- Mikutano miwili ya TAC iliitishwa (kwa robo mwaka ya kwanza na ya pili)
- Jumla ya wafanyakazi 527 walipatiwa mafunzo
- Flash disk 14 zimenunuliwa na kusambazwa kwa wahusika katika maidara.
- Powerpoint project moja (1) Overhead Screen moja (1) vimenunuliwa na kupatiwa wahusika kwa ajili ya kutumia
- Jumla ya wanafunzi 110 wa mwaka wa kwanza na wa pili wa Chuo cha Kilimo Kizimbani walipatiwa mafunzo ya UKIMWI
- Elimu ya UKIMWI kwa makundi ya Wavuvi ilitolewa katika Shehia 11 za Unguja na Pemba. Kwa Unguja Shehia hizo ni: Nungwi, Fumba, Tumbatu, Bumbwisudi, Makoba, Chwaka na Donge Muwanda na Pemba ni Chokocho, Tumbe, Furaha, Msuka na Ndagoni kwa kutumia michezo ya kuigiza:
- Wawezeshaji 130 (Unguja 70 na Pemba 60) wamepatiwa mafunzo ya wiki moja ya UKIMWI.
- Wajumbe 200 (120Unguja na 80 Pemba) wa kamati za uhifadhi wa mazingira wamepatiwa mafunzo ya UKIMWI
- Kazi ya kuingiza masuala ya UKIMWI katika mwongozo wa mafunzo ya SACCOS imefanyika kama ilivyopangwa.

**Gharama kwa mwaka 2009/2010: ni TSh.s. 30,000,000/= kutoka SMZ**

### MALENGO KWA MWAKA 2009/2010

- Kuendelea kutoa elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi wa wizara mijini na mashamba
- Kuendelea kutoa elumu kwa wadau kwa njia ya michezo ya kuigiza (community theatre shows)

## KIAMBATISHO Na. 8: MRADI SHIRIKISHI WA MAENDELEO YA KILIMO NA UWEZESHAJI PADEP

### **Maelezo mafupi ya mradi:**

PADEP ni mradi wa miaka mitano umeanza Agosti 2003. Mradi umeongezewa muda wa utekelezaji kwa miezi 18 hivyo, utafikia mwisho tarehe 30 Juni 2010. Madhumuni ya mradi huu ni kukuza maendeleo ya kilimo kwa kutoa kipaumbele utumiaji wa teknolojia zinazofaa hasa kwa walengwa kuiwezesha sekta binafsi kushiriki katika kuboresha soko la pembejeo za kilimo na mazao yanayotokana na kilimo.

**Gharama:** US \$ 4.362 million (miaka 5), 4.442 milioni (miezi 18)

**Wachangiaji (miaka 5):** 1. IDA: US \$ 3.500 milion 2. SMZ na Walengwa: US \$ 0.862 milion

**Wachangiaji (miezi 18):** 1. IDA: US \$ 3.790 milion 2. SMZ na Walengwa: US \$ 0.785 milion

**Lengo kuu:** Kujengea wakulima uwezo wakitaaluma waweze kutambua matatizo yao na kuibua miradi yao kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija na kushajiisha sekta binafsi kushiriki katika kutoa huduma za kilimo

**Gharama kwa mwaka 2008/2009:** Sh. Jumla 1,220,973,610 (Benki ya Dunia Sh. 1,180,973,610 na SMZ Sh. 50,000,000)

#### **Utekelezaji 2008/2009:**

- Tathmini ya matokeo yaliopatikana 2003/2004 -2008 imefanyika.
- Tathmini ya pamoja baina ya Benki ya Dunia na Serikali ya SMZ imeonyesha mafanikio makubwa waliopata wanajamii kwa utekelezaji wa miradi yao 574 (107 ya jamii na 467 ya vikundi vya wakulima)
- Wilaya nne mpya ambazo ni Micheweni, Mkoani, Kaskazini 'B' na Kusini zimeshajiishwa kuhusu dhana ya Mradi.
- Mafunzo ya uelewa wa mradi yametolewa kwa wawezeshaji (DMT na DFT) wapatao 66.
- Wilaya mpya zimesaidiwa kutayarisha 'Capacity Building Plan' zao na tayari mipango hiyo ya kujenga uwezo imeshawasilishwa kwa kuzingatiwa.
- Mafunzo ya Uandishi wa Miradi Midogo Midogo ya wanajamii yametolewa kwa wawezeshaji wa Wilaya ili nao wakawafunze wakulima.
- Katika kipindi cha Aprili/Juni 2009 jumla ya Sh. 682.0 milioni zinatarajiwa kutumika kugharamia miradi 31 ya jamii na 124 ya vikundi vya wakulima.

**Gharama kwa mwaka 2009/2010:** Sh. 3,746,458,000 (Benki ya Dunia Sh. 3,646,458,000 na SMZ Sh. 100,000,000).

#### **Malengo ya mwaka 2009/2010:**

- Kupeleka fedha jumla ya Shilingi 2,706.2 milioni kwa ajili ya kuekeza kwenye miradi ya jamii 47 na vikundi vya wakulima 188
- Kupeleka fedha za kujenga uwezo kwenye Wilaya mpya na kwa ajili ya kazi za ushauri na ufuatilaji kwa zile Wilaya za mwanzoni
- Kukusanya na kuweka kumbukumbu za uzoefu wa utekelezaji wa Mradi kwa matumizi ya baadae katika kusaidia maendeleo ya sekta ya kilimo
- Kufanya semina na warsha kuhusiana na masuala ya PADEP
- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wa mradi

- Kusaidia mafunzo ya Maafisa Ugani katika Chuo cha Kilimo, Kizimbani
- Kutoa mafunzo ya kilimo biashara, ujasiriamali na usarifu wa mazao ya kilimo na mifugo kwa wanajamii
- Kusaidia wanajamii kwa kuwapatia vifaa vidogo vidogo vya kusarifu na kusindika mazao
- Kufanya Warsha ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mradi Kiwilaya
- Kuandaa Warsha ya Mwisho ya Mapitio ya Mradi
- Kufanya ziara za mafunzo kwa wakulima na wawezeshaji katika maeneo ya Mradi Tanzania bara na baina ya Unguja na Pemba
- Kutayarisha Ripoti ya Mwisho ya Utekelezaji wa Mradi (ICR)
- Kuratibu na kusimamia shughuli za Mradi katika ngazi ya Shehia, Wilaya na Taifa

## KIAMBATISHO Na. 9. MRADI WA MPANGO MKUU WA UMWAGILIAJI MAJI

<b>MUDA WA MRADI 2005-2020</b>
<b>JUMLA YA GHARAMA US\$ Milioni 24</b>
<b>WACHANGIAJI - SMZ, Serikali ya Japan, Nguvu za wananchi.</b>
<b>LENGO KUU - Kuimarisha kilimo cha U/maji nchini kwa kuongeza uzalishaji, pato la wakulima wadogo wadogo na uhakika wa chakula.</b>
<b>GHARAMA KWA MWAKA 2008/2009 - 147,000,000/=</b>
<b>MALENGO YA MWAKA ULIOPITA 2008/2009</b> <ul style="list-style-type: none"><li>• Kuelimisha na kuhamasisha wakulima 4000 wa U/maji</li><li>• Kuendelea mashamba madogo madogo ya u/maji Uzini na Mgenihaji</li><li>• Kuendeleza kilimo cha uvunaji maji ya mvua</li><li>• Kuhamasisha U/maji kwa kutumia matone</li><li>• Kuwapatia mafunzo ya ndani na nje ya nchi wataalam wa Idara ya U/maji</li><li>• Ukarabati majengo ya vituo vya U/maji Cheju,B/Sudi,Mwera na Tibirinzi</li></ul>
<b>UTEKELEZAJI 2008/2009</b> <ul style="list-style-type: none"><li>• Idara imehamasisha wakulima 2,500 na kuelimisha wengine 1,500 kwa Unguja na Pemba.</li><li>• Kazi za ujenzi wa miundo mbinu ya U/maji katika maeneo ya Uzini na Mgenihaji (10ha) Matetema (2ha) na Kitogani (2ha) yako katika hatua nzuri</li><li>• Uvunaji maji umefanyika katika maeneo ya Kibokwa (20ha) ,Koani (20ha) na Kiboje (20ha) kwa Unguja na Pemba katika bonde la Weni (20ha) na Kwapweza (20ha).</li><li>• Idara imeanza utekelezaji wa kazi hii kwa kutoa mafunzo na ushauri kwa wakulima ambao wanao uwezo wa kununua vifaa kwa matumizi ya Drip Irrigation.</li><li>• Ukarabati majengo ya vituo vya U/maji katika mabonde ya Cheju , Bumbwisudi, Mwera na Tibirinzi umefanyika</li></ul>
<b>GHARAMA KWA MWAKA 2009- 2010 Sh. 180,000,000</b>
<b>MALENGO KWA MWAKA 2009-2010</b> <ul style="list-style-type: none"><li>• Ujenzi wa misingi ya saruji - 700m na misingi ya udongo - 1000m</li><li>• Ujenzi wa barabara za mashambani - 1000m</li><li>• Ujenzi wa vizingi - 50</li><li>• Uchimbaji wa visima - 2</li><li>• Ujenzi wa vibanda vya pampu - 2</li><li>• Ujenzi wa miundo mbinu ya uvunaji maji katika mashamba ya mfano</li><li>• Ukarabati wa vituo vya u/maji mashamba ya mfano</li><li>• Kusomesha wafanyakazi wa nne katika ngazi ya Diploma</li><li>• Mafunzo ya matembezi T/bara wafanyakazi 10</li><li>• Mafunzo ya wiki mbili wakulima 20 T/bara</li><li>• Mafunzo mafupi kwa wakulima 120</li><li>• Kuhamasisha na kufundisha wakulima kupitia skuli za wakulima 10</li></ul>

**KIAMBATISHO Na.10 MRADI WA MPANGO WA KILIMO CHA KISASA NA  
MAENDELEO YA KILIMO CHA UMWAGILAJI MAJI, ZANZIBAR**

<b>MUDA WA MRADI - 2007-2010</b>
<b>JUMLA YA GHARAMA - Sh. 1,550,000,000/=</b>
<b>WACHANGIAJI - Serikali , Jamhuri ya Korea na nguvu za Wananchi</b>
<b>LENGO KUU - Kuimarisha miundombinu ya kilimo cha u/maji katika bonde la Kibokwa na Bumbwisudi.</b>
<b>GHARAMA KWA MWAKA 2008/2009 - SMZ- Sh. 68,000,000/= KOICA- 1 milioni</b>

**UTEKELEZAJI 2008/2009**

- Misingi ya saruji mita 2,100 tayari imeshajengwa (mita 600 Kibokwa na mita 1,500 Bumbwisudi)
- Misingi ya udongo mita 1,000 imejengwa katika kituo cha Bumbwisudi
- Vizingi 27 vimejengwa B/sudi
- Misingi ya kutolea maji mita 600 tayari imejengwa katika kituo cha Kibokwa
- Visima sita vimechimbwa (Kibokwa - 2 na Bumbwisudi - 4)
- Visima 8 Bumbwisudi vimefanyiwa ukarabati
- Uwekaji wa pampu tayari umefanyika
- Transformer mbili za umeme mpya tayari zimeshafungwa moja katika kituo cha Kibokwa na nyengine Bumbwisudi
- Vibanda vya pampu vinane tayari vimeshajengwa, Kibokwa viwili na sita Bumbwisudi
- Afisi ndogo ya Mbweni imo katika hatua ya kuezekwa

**GHARAMA KWA MWAKA 2009- 2010**

**SMZ Sh. 180,000,000/=**

**MALENGO KWA MWAKA 2009-2010**

- Ujenzi wa misingi ya saruji - mita 800
- Ujenzi wa misingi ya udongo - mita 1500
- Ujenzi wa barabara za mashambani - mita 1,000
- Ujenzi wa vizingi - 50
- Ujenzi wa uwanja wa kuanikia mpunga Kibokwa
- Ukarabati wa Kituo cha u/maji B/sudi
- Kumalizia ujenzi wa ofisi ya U/maji Mbweni

**KIAMBATISHO Na. 11. MRADI WA MPANGO WA TAIFA WA UIMARISHAJI  
MIKARAFUU**

Muda wa mradi	Wa kuendelea
Jumla ya Gharama	
<b>Wachangiaji</b>	SMZ na Shirika la ZSTC
Lengo kuu	Kuongeza pato la wananchi kwa lengo la kupunguza umaskini
<b>Malengo maalum</b>	
<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kufufua na kuendeleza mashamba ya mikarafuu kwa kupanda miche mipyä katika maeneo yaliyowazi</li> <li>• Kufanya utafiti wa zao hilo na mazao mengine ya biashara hasa viungo, ambavyo vinaweza kuota katika mashamba ya mikarafuu.</li> </ul>	
Maeneo ya Mradi	Wilaya zote za Unguja na Pemba
<b>Vipengele vya Mradi</b>	
<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuotesha miche ya mikarafuu kwa wingi ili kutosheleza mahitaji ya wakulima</li> <li>• Kutoa elimu ya kilimo mchanganyiko cha karafuu na mazao ya viungo</li> </ul>	
<b>Gharama kwa mwaka 2008/2009</b>	
Sh. 30,000,000 kutoka SMZ.	
<b>Malengo ya mwaka 2008/2009</b>	
<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuzalisha 300,000,00 ya mikarafuu</li> <li>• Kutoa mafunzo ya kilimo mchanganyiko ya mikarafuu na mazao mengine ya viungo.</li> <li>• Kuanza matayarisho ya kuhesabu mikarafuu.</li> <li>• Kutoa mafunzo ya uchumaji na ukaushaji wa zao la karafuu.</li> </ul>	
<b>Utekelezaji 2008/2009</b>	
<ul style="list-style-type: none"> <li>• Miche 162,889 ya mikarafu imeoteshwa sawa na asilimia 54 % ya lengo.</li> <li>• Mafunzo ya kilimo mchanganyiko cha mikarafuu na mazao mengine ya viungo yametolewa kwa wakulima 550 Unguja na Pemba</li> <li>• Jumla ya wakulima 22 wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na 32 wa Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba wamepata mafunzo ya uchumaji na ukaushaji wa zao la karafuu.</li> </ul>	
<b>Gharama kwa mwaka 2009/2010</b>	
Sh. 60,000.000/= SMZ	
<b>Malengo ya mwaka 2009/2010</b>	
<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuzalisha miche 300,000 ya mikarafuu</li> <li>• Kutoa mafunzo ya ukulima bora wa mikarafuu pamoja na kuchanganya na mazao ya viungo.</li> <li>• Kufanya utafiti wa vifo vya mikarafuu midogo.</li> </ul>	

**KIAMBATISHO Na. 12: MRADI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA BAHARI  
NA UKANDA WA PWANI (MACEMP)**

<b>MUDA WA MRADI</b>	MIAKA SITA (2005 – 2011)
<b>JUMLA YA GHARAMA:</b> Shilingi bilioni 31.34 (Benki ya Dunia bilioni 25.194; Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (GEF) bilioni 5.187 na Shirika la Maendeleo la Japan (JSDF) ni shilingi milioni 959)	
<b>Lengo Kuu la Mradi</b> Kupunguza Umasikini kwa wananchi waishio katika Ukanda wa Pwani na Taifa kwa Ujumla; na kuhifadhi Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani.	
<b>Gharama za Mwaka 2008/2009:-</b> Jumla ya Dola za Kimarekani 8,922,206.00 zimepangwa kutumika (USD 6,301,863 IDA Credit: USD 2,102,043.00 GEF: USD 510,000 JSDF, na SMZ USD 8,300.00)	
<b>Utekeleza 2008/2009</b> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Jumla ya Miradi ya Jamii 195 (Pemba 105 Unguja 90) yenyewe wastani wa Shilingi bilioni tatu 3,000,000,000 imepatiwa fedha na Mradi wa MACEMP kupitia TASAF. Lengo la miaka sita la miradi ya jamii limefikiwa katika kipindi cha miaka mitatu ya mwanzo ya Mradi wa MACEMP.</li> <li>• Jumla ya miradi midogo midogo 60 imekamilishwa kupitia mfuko wa Maendeleo ya Jamii kutoka Japan (JSDF). Matumizi ya fedha za Mradi huo wa JSDF umekalika Disemba 2009.</li> <li>• Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania zimetayarishwa.</li> <li>• Utekelezaji wa Mpango wa mafunzo umeanza na jumla ya watendaji sitini (60) kutoka taasisi mbali mbali zenyewe kutekeleza Mradi wa MACEMP wamepatiwa mafunzo ndani na nje ya Nchi.</li> <li>• Ujenzi wa majengo ya afisi za maeneo tengefu (PECCA, na MENAI) tayari umeanza huko Kizimkazi hapa Unguja na Wesha huko Pemba. Aidha, matayarisho yote ya Ujenzi wa eneo la MIMCA yamekamilishwa na ujenzi kwa eneo hilo utaanza mara utaratibu wa kupata eneo na kupimwa utakapomalizika.</li> <li>• Uchoraji wa michoro na ramani za Ujenzi wa afisi za Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania litakalojengwa kisiwani Zanzibar katika eneo la Fumba upo katika hatua za mwishoni.</li> <li>• Michoro kwa Ujenzi wa afisi mbili za Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini Unguja na Pemba imekamilika.</li> <li>• Idara ya Mazingira imeendelea kuwezeshwaa kuweza kuendeleza matayarisho ya mpango wa usimamizi shirikishi wa rasilimali za Bahari na Ukanda wa Pwani.</li> <li>• Kazi ya matayarisho ya mpango mkuu wa utekelezaji wa maeneo tengefu utaanza hivi karibuni baada ya kupatikana mtaalam wa kufanya kazi hio.</li> <li>• Utafiti wa bioanuai kwa eneo la Tumbatu na visiwa vya Mji Mkongwe (Bawe, Prison nk) umeanza kwa mafanikio makubwa.</li> <li>• Kuwezesha taasisi za Idara ya Uvuvi, Idara ya Mazingira, Misitu, Mambo ya kale, Ardhi na Mipango Miji, Kamisheni ya Utalii kuendeleza kazi zao chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa MACEMP.</li> <li>• Kukamilisha kazi ya matayarisho ya Mpango wa Usimamizi wa Misitu ya Mikoko.</li> </ul>	
<b>Jumla U\$D 8,107,001.00 zimepangwa kutumika katika mwaka 2009/2010 kutoka IDA na kutoka SMZ Sh. 100,000,000 zimepangwa kutumika</b>	

**Malengo ya Mwaka 2009/2010:**

- Kuongeza kasi ya kutoa miradi kwa jamii kwa Unguja na Pemba. Aidha jumla ya shilingi bilioni moja itatumika na miradi 100 ya ziada inategemewa kutekelezwa ambapo miradi (50 Unguja na 50 Pemba). Hatua hii itafikisha miradi 340 ya jamii kupitia fedha za MACEMP kwa utaratibu wa TASAF.
- Kuendelea kutoa taaluma kwa wakulima wa mwani 7000 na wavuvi 8000 wa ukanda wa Pwani kwa visiwa vya Unguja na Pemba katika kutekeleza Uvuvi na Ukulima wa Mwani Bora wenye faida kubwa. Aidha, utafiti wa ukulima wa mwani wa Cotonii katika maji marefu utakamilishwa.
- Kukamilisha Ujenzi wa afisi za PECCA, MIMCA na MBCA.
- Kuanza na kukamilisha Ujenzi wa afisi za Idara ya Uvuvi kwa Unguja na Pemba.
- Kuanza kwa ujenzi wa afisi za Mamlaka ya Uvuvi wa bahari kuu Tanzania zitakazojengwa Fumba - Zanzibar.
- Kuanza kwa ujenzi wa soko la Tumbe Kisiwani Pemba na ujenzi wa Soko na Maabara - Unguja.
- Kuanza ukarabati wa Maeneo matatu ya Kihistoria (Palace Museum, Beit el ajab na Mtoni Palace). Aidha, maeneo mengine 25 kwa Unguja na Pemba yatapimwa na taarifa zake kuhifadhiwa kwa matumizi ya vizazi vya hivi sasa na vizazi vijavyo.
- Kufadhili masomo kwa wataalam 100 ndani na nje ya nchi.
- Kukamilisha mchakato wa kuanzishwa kwa mamlaka ya Uvuvi wa Bahari kuu Tanzania.
- Kukamilisha utafiti wa Bioanuai wa maeneo ya Hifadhi ya Tumbatu na visiwa vya Mji Mkongwe (Bawe, Chumbe na Prison).
- Kushirikiana na jamii kwa kuendelea kusimamia Uhifadhi wa Maeneo ya PECCA, MIMCA na MENAI.
- Kukamilisha utafiti wa uwezo wa maeneo ya hifadhi na kiwango cha watalii ambaao wanawenza kutembelea bila kuathiri mazingira.
- Kutangaza mafanikio ya Mradi wa MACEMP ndani na nje ya Nchi pamoja na kuanza utaratibu wa kuanzishwa kwa MACEMP II ili kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa.

**KIAMBATISHO Na. 13. TAARIFA YA MAPATO**

<b>TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MAPATO KUANZIA JULAI,08 HADI APRIL,09 PAMOJA NA MAKISIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2009/2010</b>					
<b>KASMA</b>	<b>CHANZO CHA MAPATO</b>	<b>MAKADIRIO YA MWAKA 2008/2009</b>	<b>FEDHA ZIZLIZO KUSANYWA KUANZIA JULAI,08 HADI APRIL,09</b>	<b>SAWA NA ASILIMIA</b>	<b>MUSWADA WA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA 2009/2010</b>
37044	MAPATO MENGINEYO	285,200,000.00	828,290,835.00	290.42	966,370,000.00
34018	ADA YA UINGIZAJI WATALII	10,000,000.00	1,457,500.00	14.58	2,000,000.00
37012	UKAGUZI WA MAZAO	16,600,000.00	7,662,000.00	46.16	17,900,000.00
37015	MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE	10,600,000.00	5,613,500.00	52.96	11,000,000.00
37018	MAUZAJI YA MBOLEA	12,000,000.00	-	0.00	-
37020	UTIBABU WA VINYAMA	35,000,000.00	39,905,230.00	114.01	56,000,000.00
28001	MAZAO YA MISITU	132,000,000.00	105,478,791.00	79.91	157,000,000.00
28002	ADA YA UUZAJI WA MAWE MCHANGA, KOKOTO	97,000,000.00	67,138,020.00	69.21	123,000,000.00
37062	MAUZO YA MICHE	15,130,000.00	4,609,100.00	30.46	15,130,000.00
32006	LESENI ZA UVUVI	14,400,000.00	9,001,300.00	62.51	14,500,000.00
32007	MAZAO YA BAHARINI	56,000,000.00	23,104,780.00	41.26	48,000,000.00
37095	ADA YA HIFADHI YA MAZINGIRA	6,447,000.00	58,500.00	0.91	10,000,000.00
37096	ADA YA UKAGUZI WA MAZIGIRA	2,625,000.00	2,060,000.00	78.48	3,000,000.00
35015	ADA YA UANDIKISHAJI WA VYAMA	1,700,000.00	3,309,000.00	194.65	4,000,000.00
35016	ADA YA UKAGUZI WA VYAMA	2,000,000.00	1,242,000.00	62.10	2,000,000.00
<b>JUMLA KUU</b>		<b>696,702,000.00</b>	<b>1,098,930,556.00</b>	<b>157.73</b>	<b>1,429,900,000.00</b>

**KIAMBATISHO Na. 14: TAARIFA ZA KAZI ZA MIRADI YA MAENDELEO**

**FEDHA ZIZLIZOTOLEWA KWA KAZI ZA MAENDELEO KUANZIA JULAI,2008 HADI APRIL,2009**

KASMA	MAELEZO	MAKISIO YA MWAKA 2008/2009	FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI,8 HADI APRIL,09	SAWA NA ASILIM	MAPENDEKEZO YA MWAKA 2009/2010
	<b>IDARA YA SERA NA MIPANGO</b>				
61205	PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO MIFUGO (ASDPL)	55,000,000.00	55,000,000.00	100.00	100,000,000.00
61225	PROGRAMU YA KUIMARISHA HUDUMA ZA KILIMO (ASSP)	185,000,000.00	150,180,242.00	81.18	360,000,000.00
61300	PROGRAMU YA KUELIMISHA WADAU WA SEKTA YA KILIMO – UKIMWI	15,000,000.00	8,500,000.00	56.67	30,000,000.00
61310	MRADI WA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE	64,000,000.00	59,000,000.00	92.19	160,000,000.00
61320	MRADI WA KUKUZA USARIFU WA MAZAO YA KILIMO	25,000,000.00	15,593,600.00	62.37	170,000,000.00
	<b>KAMISHENI YA KILIMO,UTAFITI NA ELIMU KWA WAKULIMA</b>				
61260	MRADI WA USHIRIKISHWAJI WA MAENDELEO YA KILIMO (PADEP)	50,000,000.00	50,000,000.00	100.00	100,000,000.00
	<b>IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO</b>				
61206	MRADI WA KUTHIBITI KICHAACHA MBWA	10,000,000.00	8,000,000.00	80.00	25,000,000.00
61207	MRADI WA UPANDISHAJI NGOMBE KWA SHINDANO	508,000,000.00	107,000,000.00	21.06	40,000,000.00
	<b>IDARA YA MAZAO YA BIASHARA,MATUNDA NA MISITU</b>				
61240	MRADI WA KUIMARISHA MIKARAFUU	30,000,000.00	17,436,019.20	58.12	60,000,000.00
61250	PROGRAMU YA UWIANO NA USIMAMIZI WA MALIASILI	113,000,000.00	92,390,320.10	81.76	-
	<b>IDARA YA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI</b>				
61270	MRADI WA GHUBA YA MINAI	20,000,000.00	17,000,000.00	85.00	30,000,000.00
61290	MRADI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA U/PWANI (MACEMP)	10,000,000.00	10,000,000.00	100.00	100,000,000.00
	<b>IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI</b>				
61215	MPANGO MKUU WA MAENDELEO YA KILIMO CHA U/MAJI	147,000,000.00	53,378,139.00	36.31	180,000,000.00
61216	MRADI WA KILIMO CHA KISASA NA UENDELEZAJI WA KILIMO CHA U/MAJI	68,000,000.00	59,345,000.00	87.27	180,000,000.00
	<b>JUMLA YA MIRADI MIKONGWE</b>	<b>1,300,000,000.00</b>	<b>702,823,320.30</b>	<b>54.06</b>	<b>1,535,000,000.00</b>
	<b>MIRADI MIPYA</b>				
	<b>IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO</b>				
	MAFUA YA NDEGE				<b>50,000,000.00</b>
	<b>IDARA YA MAZINGIRA</b>				
	PROGRAMU YA KUHFADHI MAZINGIRA YA UKANDA WA PWANI (INA MIRADI MITATU – ReCoMaP, MCA-T na Mradi wa Msingini Pemba)				<b>40,000,000.00</b>
	<b>IDARA YA VYAMA VYA USHIRIKA</b>				
	PROGRAMU YA MAENDELEO YA USHRIKA				<b>25,000,000.00</b>
	<b>JUMLA KUU</b>				<b>1,650,000,000.00</b>